UCHANGANUZI WA MAUDHUI YA NYIMBO ZA MSONDO NA ATHARI ZAKE KWA WANANDOA KATIKA JAMII YA WADIGO

UMI SALIM KAOLE

TASNIFU HII IMEWASILISHWA KWA AJILI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU CHA PWANI.

MEI, 2018

UNGAMO NA IDHINI

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa katika chuo kikuu kingine chochote.

Sahihi _____ Tarehe 18·10·2018

UMI SALIM

C50/1B/2218/2013.

IDHINI

Tunathibitisha kwamba kazi iliyowasilishwa katika tasnifu hii ya shahada ya uzamili ilifanywa na mtahiniwa mwenyewe chini ya usimamizi wetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Pwani.

Sahihi _____ Tarehe 18·10·2018

Prof. Rocha Chimerah

Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi, Chuo Kikuu Cha Pwani.

Sahihi _____ **Tarehe** 18.10.2018

Prof. Furaha Chai

Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi, Chuo Kikuu Cha Pwani.

TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia familia yangu, wanangu wapendwa Yusuf na Yusra na marehemu mwanafunzi mwenza Emmanuel Chai. Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi.

SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, afya njema na nguvu za kuniwezesha kukamilisha masomo yangu ya uzamili, sifa njema zote ni zake.

Kwanza nawashukuru wazazi wangu kwa kunilea na kunipa nafasi ya kupata elimu hadi kufikia kiwango hiki cha uzamili.

Nawashukuru wasimamizi wangu Prof. Chimerah na Prof. Chai waliojitolea na kutumia muda wao na kwa uvumilivu kusoma na kunielekeza na kunipa ushauri mwema hadi kufikia mwisho wa kumaliza kazi hii. Nitawashukuru daima na kuwatakia heri njema na baraka.

Shukrani zangu za dhati kwa wahadhiri wa idara ya Kiswahili walionifunza wakiwemo marehemu Prof.Stephen Karisa Beja (Mungu ailaze roho yake mahali pema), Dkt. Nancy Ngowa na Dkt Rukia. Mungu awabariki kwa usaidizi wenu.

Nawashukuru wanafunzi wenzangu Bw. Enos Mwaruka, Bi. Shekha na Bw. Chembea kwa kunipa moyo na kushirikiana nami katika masomo haya ya uzamili hadi kuhitimu kwetu.

Mwishowe nawashukuru wale wote walionisaidia nyanjani wakati wa kukusanya data ya kufanikisha utafiti huu.

IKISIRI

Nyimbo za msondo za jamii ya Wadigo ni aina za nyimbo ambazo huimbwa wakati wa harusi upande wa kwa bi. harusi na huwa tofauti kabisa na nyimbo za harusi za kawaida. Utafiti huu ulinuia kuchanganua maudhui ya nyimbo za msondo na athari zake kwa wanandoa katika jamii ya Wadigo. Malengo matatu yaliongoza utafiti huu yakiwemo kuchanganua maudhui yanayojitokeza katika nyimbo hizi za msondo, kubainisha miiko inayofungamanishwa na nyimbo hizi na kubainisha athari zinazohusishwa na nyimbo hizi za msondo. Ili kutimiza malengo haya mtafiti aliongozwa na nadharia ya uhalisia kwani maudhui ya nyimbo za msondo na athari zake zinahusishwa na utamaduni wa mila ya jamii ya Wadigo ambayo hufungamana na maisha yao ya kila siku. Nadharia hii ilitumika katika utafiti huu kwa sababu inashikilia kwamba hali zote za maisha ya kijamii hustahili kuelezwa katika uhalisi wake kama unavyoonekana wala sivyo unavyofikiriwa kuwa. Utafiti huu ni wa kithamano huku ukizingatia muundo wa kimaelezo. Mbinu za uchunguzi shirikishi katika miktadha isiyo rasmi na mahojiano zilitumika katika ukusanyaji wa data. Data zilikusanywa kutoka nyanjani ambapo mtafiti alionana ana kwa ana na watafitiwa. Sampuli ya kimaksudi ilitumika kuteua mshiriki mmoja ambaye alisaidia katika uteuzi wa washiriki wengine kupitia sampuli tajwa. Sampuli hii ili jumlisha watu hamsini wakiwemo makungwi, wanawake waliochezewa nyimbo za msondo, wanawake ambao hawakuchezewa nyimbo za msondo na wanaume waliopo katika ndoa ili kutoa maoni yao kuhusiana na mafunzo ya nyimbo hizi. Data hii ilichanganuliwa na kuwasilishwa kutumia grafu ambapo asilimia ya watafitiwa ndio iliyotumika kuelezea maoni ya wanajamii kuhusiana na mada hii ya utafiti. Utafiti huu utatoa mchango wa kueleza utamaduni, mila na desturi za jamii ya Wadigo na kuweka wazi masuala ya nyimbo hizi za msondo kiakademia. Utafiti huu vilevile utachangia katika hazina ya maswala ya fasihi simulizi ya Afrika.

YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINI ii

TABARUKU iii

SHUKRANI.....iv

IKISIRI.....v

YALIYOMO. vi

MAELEZO YA ISTILAHI.....x

SURA YA KWANZA UTANGULIZI. 1

1.1 Usuli wa mada. 1

1.2 Swala la utafiti. 3

1.3 Malengo ya utafiti. 3

1.4 Maswali ya utafiti. 3

1.5 Sababu za kuchagua mada. 4

1.6 Umuhimu wa utafiti.....4

1.7 Upeo na mipaka.....5

1.8 Udhaifu wa utafiti.....6

SURA YA PILI UHAKIKI WA MAANDIKO. 7

2.1 Utangulizi 7

2.2 Yaliyoandikwa kuhusu mada 7

2.3 Msingi wa nadharia 11

2.3.1 Mihimili ya nadharia ya uhalisia katika uchanganuzi wa nyimbo za msondo. 13

SURA YA TATU MBINU ZA UTAFITI 16

3.1 Utangulizi 16

3.2 Eneo la utafiti 16

3.3 Mbinu za utafiti 16

3.4 Uteuzi wa sampuli 17

3.5 Mbinu za kukusanya data 18

3.6 Mbinu za uchanganuzi wa data 19

3.7 Uwasilishaji wa data 20

SURA YA NNE UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA.....21

4.1 Utangulizi. 21

4.2 Uchambuzi wa maudhui ya nyimbo za msondo 21

4.3 Uchambuzi wa maudhui ya nyimbo za msondo yanayohusu unyumba. 23

4.3.1 Kuonyesha nafasi ya ndoa katika jamii. 24

4.3.2. Kuonyesha umuhimu wa tendo la ndoa. 24

4.3.3 Kuonyesha mitindo tofauti ya ngono. 26

4.3.4 Nafasi ya mwanamke katika ndoa 28

4.3.5 Uke wenza katika jamii. 28

4.3.6 Kupeana vijembe 29

4.3.7 Kusifu na Kukashifu matendo. 30

4.3.8 Utunzaji wa siri katika ndoa. 31

4.4. Uchambuzi wa maudhui ya nyimbo za msondo yasiyohusiana na unyumba. 32

4.4.1 Kuonyesha nafasi ya Mungu katika jamii. 32

4.4.2 Kuimarisha mila na desturi 32

4.4.3 Kupeana tahadhari 33

4.4.4 Kitambulisho cha jamii 34

4.4.5 Kuburudisha 34

4.5 Uchambuzi wa miiko inayofungamanishwa na nyimbo za msondo. 35

4.5.1. Uhusika katika nyimbo za msondo. 37

4.5.2. Vyeo vya wahusika wa msondo. 38

4.5.3 Dhana ya Kisima 39

4.5.4 Ngoma za msondo 40

4.5.5 Kanuni ya mavazi 40

4.5.6 Matendo katika msondo 41

4.5.7 Mizungu.....41

4.5.8 Ada za msondo 42

4.6 Uchambuzi wa athari ya nyimbo za msondo katika jamii.....42

4.7 Athari chaya zinazohusishwa na nyimbo za msondo 44

4.7.1. Kuhifadhi historia 44

4.7.2 Kudumisha mila na desturi 45

4.7.3 Ushirikiano katika jamii 46

4.7.4 Kufunza maadili katika ndoa.....46

4.7.4.1 Kuheshimu ndoa 47

4.7.4.2 Uvumilivu katika majukumu mazito ya ndoa 47

4.7.4.3 Kumridhisha mume 48

4.7.4.4 Usafi 48

4.7.4.5 Sauti ya mwanamke.....50

4.7.4.6 Uvivu 50

4.7.4.7 Shanga za kiunoni 51

4.7.4.8 Kuzuia kuenea kwa utandawazi 52

4.8 Athari hasi zinazohusishwa na nyimbo za msondo.....53

4.8.1 Ukosefu wa maadili.....53

4.8.2 Nyimbo za matusi.....53

4.8.3 Mavazi ya nyimbo za msondo.....54

4.8.4 Uasherati.....54

4.8.5 Athari ya usagaji.....55

4.8.6 Ushirikina.....55

4.8.7 Udhalilishaji wa wanawake.....56

4.8.8 Uharibifu wa mali.....57

4.8.9 Masuala ya kidini.....58

4.8.10 Utengano katika jamii.....59

4.8.11 Kuzuka kwa tamaduni ya ‘kitchen party’.....60

SURA YA TANO MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO. 63

5.1 Utangulizi.....63

5.2 Mukhtasari wa tasnifu.....63

5.3 Mukhtasari wa matokeo.....64

5.4 Hitimisho.....65

5.5 Mapendekezo.....67

MAREJELEO.....70

KIAMBATISHO CHA 1.....73

MWONGOZO WA MAHOJIANO.....73

KIAMBATANISHO 2.....75

NYIMBO.....75

MAELEZO YA ISTILAHI

Bi……..	Bibi
Dufu……	Aina ya nyimbo za harusi kwa maadili ya Kiislamu
Kimuhakati …….	Usimulizi wa matukio kama yanavyotokea katika ulimwengu.
Kuinikwa……..	Mafunzo yanayohusishwa na ndoa
Kungwi ……..	Mwanamke anayewafunza mabinti mambo ya unyumba.
Kuregua…….	Kufungua shanga kwa mdomo
Kushenga……..	Usafi wa sehemu za siri
Kusinga…….	Kumuosha mume au mke
Maharimu……..….	Mtu usiyeweza kumuoa au kuolewa naye
Makumbakusenge……	Chama cha msondo
Mizungu……	Mbinu za kucheza
Mkurugwa……	Kungwi mkubwa
Msondo……..	Ngoma ndefu
Mwari……	Msichana anayetaka kuolewa
Myugwa……..	Aina ya fimbo inayoyumbuka
Nyimbo za Msondo……..	Nyimbo zinazoimbwa wakati wa harusi upande wa bi. harusi
Omo…….	Chama cha msondo
Shangingi……	Mwanamke hodari wa maswala ya unyumba
Sogoro……..	Mwanamke anayepiga ngoma za msondo
Somu ……	Mwanamke anayefundisha mambo ya unyumba
TUKI ……..	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Uhalisia ……..	Kueleza hali au jambo jinsi lilivyo kwa uamilifu.
Ushabihikweli …….	Kuukaribia ukweli uliopo katika jamii.
Visutu (ndwambwi)……	Aina za leso
Vumi…….	Aina ya ngoma iliyo fupi

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Mada

Nyimbo za msondo hupatikana katika jamii ya Wadigo ambao ni miongoni mwa makabila tisa yanayounda kundi la Wamijikenda. Wadigo wanapatikana katika kaunti ya Mombasa na wengi wao wakipatikana katika kaunti ya Kwale. Nyimbo hizi za msondo huimbwa wakati wa harusi na huwa tofauti na nyimbo za harusi za kawaida. Mambo mengi kuhusiana na utaratibu, maudhui ya nyimbo za harusi hujulikana na wanajamii lakini wanajamii wachache sana ndio hujua kuhusu nyimbo hizi za msondo. Hali hii ndiyo ilimfanya mtafiti kutaka kuziba pengo hili kwa kuchanganua maudhui, miiko na athari zilizotokana na nyimbo hizi za msondo.

Kulingana na Spear (1978), asili ya Wamijikenda ni Singwaya katika bonde la mto Juba. Inadaiwa Wamijikenda walikuwa wakiishi pamoja huko Singwaya na wakashambuliwa na Wagalla hali hii ilisababisha Wadigo kuondoka kwanza kuelekea pwani hadi Shimba Hills, kusini Magharibi mwa Mombasa ambapo walianzisha kaya Kwale, na baadhi yao wakaanzisha kaya Kinondo. Kutokana na kaya hizi mbili, vikundi vidogo vidogo viliondoka na kwenda kuanzisha kaya zingine ndogondogo. Kwa mujibu wa Spear (1978), Mijikenda ni wakulima na wafugaji tangu walipokuwa Singwaya. Mbali na kilimo, Wadigo walijihusisha na biashara na walifanya biashara hizi na Waswahili na hali hii ilisababisha mwingiliano kati ya jamii hizi mbili.

Mwingiliano mkubwa zaidi ni wa kidini na kwa sababu hii Wadigo wengi ni wafuasi wa dini ya Kiislamu na hufuata desturi za dini hii kupitia mavazi, shughuli za harusi, salamu, shughuli za mazishi na nyinginezo. Kulingana na mwingiliano huu wa jamii hii ya Kidigo na dini ya Kiislamu tunaona ya kwamba jamii hii hufanya harusi kuzingatia mielekeo miwili. Mmoja ni kwa kuzingatia kanuni ya dini ya kiislamu ambapo hakuna nyimbo za

msondo na mwelekeo wa pili ni kufuata tamaduni za Wadigo ambapo huwepo nyimbo za msondo katika sherehe ya harusi.

Kulingana na Matei (2011), nyimbo ni tungo za kishairi zenye mahadhi ya kupanda na kushuka kwa sauti, muwala na mapigo ya kimuziki na huwasilishwa kwa kuimbwa. Nyimbo hutambuliwa kwa sifa tatu; kuwepo kwa hadhira inayotumbuizwa, muziki unaoimbwa kwa sauti na matumizi ya ala.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), nyimbo ni tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka. Tungo hizi huundwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya picha na mapigo ya silabi na hupangwa kwa utaratibu au muwala wenye mapigo ya kimuziki au mizani. Nyimbo huchukua sehemu kubwa katika miviga ya jamii mbalimbali.

Nyimbo hizi za msondo hutumia mapigo ya ngoma kuashiria maana tofauti tofauti na hujulikana na wapigaji wa ngoma hizi au watu wazima wanajua milio hiyo humaanisha nini. Nyimbo za msondo huimbiwa mabibi harusi pekee na ni nyimbo zinazoimbwa kwa upande wa bi. harusi pekee na tunaweza kuhusisha ngoma hizi za msondo na unyago.

TUKI (1981), inafasili unyago kuwa ni mkutano wa watu maalumu, mahali maalumu pa siri panapofundishwa mizungu ya mila za kabila kwa vijana. Au ni ngoma ya kuwafundisha wari mila za kabila lao.

Katika jamii ya Wadigo, nyimbo hizi za msondo hutumiwa kuwafundisha watoto wa kike mambo ya unyumba na unyago. Mawazo kama haya yanatolewa na mwana muziki wa Taarab, Bi. Kidude kutoka Zanzibar (2013:2), aliyesema kwamba, ‘aliwafundisha wanawake wachanga wa Waswahili kuhusu kubalekhe, jinsi ya kuishi na waume zao na kupiga vita udhalilishaji wa kijinsia na kihadhi’’. Kupitia nyimbo hizi mafunzo haya yalifanywa kupitia kwa mapigo ya ngoma za kitamaduni zikiambatanishwa na uchezaji wa ngoma.

Nyimbo hizi za msondo katika jamii ya Wadigo hazichezwi hadharani kwa sababu inasemekana ni mambo ya siri yanayoonyeshwa bibi harusi na huchezewa chumbani na wanawake mahususi. Sio kila mwanamke aliyehudhuria sherehe hizo za harusi huingia chumba hicho kuimba na kucheza nyimbo za msondo ni baadhi tu kama vile wanachama wa msondo, makungwi, wari waliochezewa nyimbo za msondo na mashangazi wa bi. harusi ambao ni watu wazima wanayoyafahamu mambo ya unyumba.

1.2 Swala la Utafiti

Nyimbo za msondo ni za kipekee na hupigwa na kuchezwa wakati wa harusi mahali ambapo bi. harusi hupatikana na huwa tofauti na nyimbo za harusi za kawaida. Ingawa tafiti mbalimbali zimewahi kufanywa kuhusiana na nyimbo za harusi. Hata hivyo swala la ni maudhui gani nyimbo hizi huangazia na athari zake kwa wanajamii halijashughulikiwa katika maandishi ya kiakademia.

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una malengo yafuatayo:

i) Kuchanganua maudhui yaliyojitokeza katika nyimbo teule za msondo za jamii ya Wadigo.

ii) Kubainisha miiko iliyofungamanishwa na nyimbo hizi za msondo.

iii) Kubainisha athari zilizojitokeza kutokana na nyimbo hizi za msondo.

1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

i) Nyimbo za msondo zina maudhui gani?

ii) Kuna miiko gani iliyohusishwa na nyimbo hizi za msondo?

iii) Kuna athari gani zilizojitokeza katika jamii ambazo hutokana na maudhui ya nyimbo za msondo?

1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Uchaguzi wa mada hii ya utafiti ulitokana na kuwa watafiti wengi wamechanganua aina za nyimbo mbalimbali za harusi kama vile nyimbo za harusi za Waswahili, Wakamba, Wadigo lakini hakuna taarifa ya maswala ya nyimbo za msondo yaliyoelezewa kiakademia kuhusu jamii ya Wadigo.

Mtafiti anahamu ya kuweka wazi maswala ya utamaduni wa Wadigo ambayo hayajafafanuliwa kwa kirefu ilhali ni mambo yanayotokea katika jamii hii. Wanajamii wanajihusisha sana na nyimbo za harusi za kawaida ilhali kuna nyimbo za kipekee za harusi zinazoitwa nyimbo za msondo ambazo iwapo maswala yake hayatajadiliwa na kuwekwa wazi basi nyimbo hizi zitapotea. Kwa hivyo mtafiti alitaka kuziba pengo hili kwa kuonyesha tofauti kati ya nyimbo za kawaida za harusi na nyimbo hizi za msondo katika jamii ya Wadigo

Vilevile kuna haja ya kubainisha umuhimu wa nyimbo hizi katika sherehe za harusi na athari zake katika jamii, kwani sio kila harusi ambapo kutakuwepo na nyimbo hizi za msondo. Ni baadhi tu ya harusi ambapo bi. harusi huimbiwa na kuchezewa nyimbo hizi za msondo.

Nyimbo nyingi za harusi hujumlisha jamii nzima wakiwemo wanawake na wanaume lakini nyimbo hizi za msondo huimbwa na wanawake pekee katika jamii hii na kuwatenga wanaume. Kwa hivyo mtafiti alitaka kujua sababu ya wanaume kutoruhusiwa kuingia au kuimba na kutohusishwa kabisa na nyimbo hizi za msondo.

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utachangia katika hazina ya maswala ya fasihi ya Kiafrika na matokeo yake yataweza kuwekwa katika hazina ya mafundisho ya utamaduni wa jamii ya Wadigo ambayo yatawanufaisha wengine katika tamaduni zitakazopata usomi huu.

Vilevile utafiti huu utawasaidia wataalamu wa fasihi kama vile maprofessa, wahadhiri, walimu na wanafunzi kupata data zinazohusu nyimbo za ngoma ya msondo. Watafiti wengine watakaohitaji kufanya utafiti katika uwanja huu wa nyimbo watapata kianzishio kwa kusoma utafiti huu.

Utafiti huu utasaidia kuhifadhi mila na utamaduni wa jamii ya Wadigo katika maandishi kwani mambo mengi ya simulizi ya fasihi bado yamehifadhiwa vichwani mwa watu kama sehemu ya kutunza utamaduni huu.

Utafiti huu wa nyimbo za msondo una umuhimu kwani matokeo ya utafiti huu yataonyesha mwelekeo kwa jamii ya Wadigo, iwapo elimu hii inayotokana na nyimbo za msondo inafaa kudumishwa, kurekebishwa au kutupiliwa mbali. Hii ni kwa sababu maudhui ya nyimbo za msondo yanahusishwa na dhana nyingi potovu. Utafiti huu utasaidia kujua ukweli uliopo kuhusiana na nyimbo za msondo.

1.7 Upeo na Mipaka

Nyimbo za harusi ni nyingi katika jamii tofauti na zimefanyiwa utafiti na watafiti mbalimbali kwa hivyo mtafiti alijikita katika nyimbo za harusi za msondo. Nyimbo hizi za msondo vilevile zinajitokeza katika jamii mbalimbali kama vile jamii ya Wabajuni na Wapemba lakini mtafiti ametafiti nyimbo za msondo za jamii ya Wadigo pekee.

Jamii ya Wadigo wanapatikana katika sehemu mbalimbali za pwani kama vile Likoni, Shikaadabu, Waa, Ng’ombeni, Tiwi, Kombani na kadhalika. Jamii hizi zinaishi katika sehemu tofauti tofauti za pwani na ingekuwa gharama kubwa kufanya utafiti katika sehemu zote wanazopatikana Wadigo. Kwa sababu hii, utafiti huu ulijikita katika nyimbo za msondo za jamii ya Wadigo wa Likoni pekee hususan mitaa ya Jamvi la Wageni na Migombani ambao wameathirika sana na lugha ya Kiswahili. Tukizingatia nyimbo zilizokusanywa tuligundua ya kwamba kuna athari ya lugha ya Kiswahili katika nyimbo hizi ilhali tulizingatia jamii ya Wadigo ambao lugha yao ni Kidigo.

Mtafiti alichambua nyimbo kumi na nane ambazo zilijulikana sana na watafitiwa na kuelezea maana na umuhimu wake ilhali kuna nyimbo nyingi ambazo huimbwa wakati wa sherehe hizi za msondo. Mtafiti alichagua nyimbo hizi kwa sababu nyimbo nyingi zilikuwa zinazungumza maudhui sawa kwa hivyo mtafiti alichagua zile nyimbo tofauti zilizozungumzia maudhui tofauti.

1.8 Udhaifu wa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika mitaa miwili pekee ilhali nyimbo hizi za msondo huimbwa na jamii nzima ya Wadigo katika sehemu tofauti tofauti.

Ngoma za msondo hupigwa na nyimbo zake huimbwa wakati wa sherehe za harusi. Changamoto ni kuwa sio kila sherehe ya harusi ambapo kulikuwa na ngoma na nyimbo hizi za msondo, kwa sababu maswala ya nyimbo hizi ni ya utamaduni wa Wadigo na wanajamii wengi wanafuata dini ya Kislamu na husherekea harusi kwa misingi ya dini hii na kuachilia mbali utamaduni huu wa kuimba nyimbo za msondo. Kwa hivyo ilimbidi mtafiti kutafuta na kusubiria harusi iliyofanyika ambapo kuliimbwa na kuchezwa nyimbo hizi za msondo.

Mtafiti alihitaji kuwahoji makungwi, wanawake waliochezewa msondo, wanawake ambao hawakuchezewa msondo na wanaume waliomo ndani ya ndoa. Watafitiwa hawa walitoa maelezo kutokana na tajriba zao kuhusiana na maswala ya nyimbo hizi za msondo.

Mwishowe nyimbo hizi huimbwa na kuchezwa na wanawake pekee, kuna wanawake wanaoitwa makungwi ambao ndio wahusika wakuu katika nyimbo hizi, kuwapata wanawake hawa na kuwahoji ilikuwa changamoto kubwa. Hii ni kwa sababu ya dhana kwamba mambo wanayoyafanya ni mwiko kuelezwa kwa watu ambao hawahusiki moja kwa moja na nyimbo hizi za msondo.

SURA YA PILI

UHAKIKI WA MAANDIKO

2.1 Utangulizi

Watafiti wengi wameshughulikia utanzu wa nyimbo katika jamii tofauti kama nyimbo za harusi za jamii ya Wadawida, Waswahili, Wadigo na jamii nyengine nyingi. Kazi zao zilimnufaisha mtafiti kwa kuangazia masuala waliyotafiti kama vile maudhui, majukumu na athari za nyimbo hizi. Mtafiti aliweza kuelezea mfanano na tofauti ya tafiti hizo na utafiti huu na vile vile kukubaliana na baadhi ya matokeo yaliyopatikana katika tafiti hizo.

2.2 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Mogambi (2007), alishughulikia nyimbo kwa jumla na aliangalia dhima, maudhui na sifa za nyimbo. Kazi hii ilimuongoza mtafiti katika uchambuzi wa maudhui yanayopatikana hasa katika nyimbo za msondo tukiona ya kwamba baadhi ya maudhui aliyoyaainisha yalijitokeza katika nyimbo za msondo kama vile kufunza maadili, kuhifadhi mila na desturi za jamii na kuburudisha. Hata hivyo utafiti wake ulitofautiana na wetu kwani hatukuangazia sifa za nyimbo za msondo.

Kirubi, Ngonje na Wandeo (2007), walishughulikia nyimbo kwa jumla. Waliangalia dhana ya nyimbo, sifa, muundo, aina na majukumu tofauti tofauti ya nyimbo. Kazi hii ilimfaa mtafiti kwani kati ya aina za nyimbo zilizoorodheshwa kulikuwa na nyimbo za unyango ambazo tunazinasibisha na nyimbo hizi za msondo. Vilevile walishughulikia majukumu ya nyimbo kwa jumla na tukilinganisha majukumu hayo na ya nyimbo za msondo tulipata baadhi ya majukumu bado ni yale yale kama vile kuhifadhi mila na desturi , kuelimisha na kuburudisha.

Beja (2000), alielezea kuhusu tamaduni za mijikenda ambapo nyimbo hutumika na kueleza aina mbalimbali za nyimbo kama vile kifudu na mwandzelle alipokua anaelezea kuhusu utaratibu wa nyimbo za matanga. Kazi hii ilimsaidia mtafiti katika kueleza vipengele

vilivyozingatiwa wakati wa kuangazia maudhui yaliyojitokeza katika nyimbo. Hata hivyo, utafiti wetu ulitofautiana na kazi hii kwani tulishughulika na uchunguzi wa nyimbo za msondo za jamii ya Wadigo na wala sio nyimbo za matanga katika jamii ya Wagiriama.

Timammy (2002), ambaye aliangazia shughuli za harusi ya Waswahili na utaratibu wake kuanzia posa hadi ndoa na kuchambua nyimbo za Waswahili kuzingatia mtindo wa nyimbo hizi za harusi. Kazi hii ilimsaidia mtafiti katika kuchambua nyimbo za msondo kwani nyimbo hizi vilevile huwa na mtindo tofauti tofauti kulingana na mapigo yake ya ngoma wakati wa sherehe ya harusi. Hata hivyo utafiti huu ni tofauti kwani tulizingatia maudhui, miiko na athari za nyimbo za msondo wa jamii ya Wadigo.

Mjomba (2011), alitafiti kuhusu nyimbo za harusi katika jamii ya Wadawida. Utafiti wake ulijikita katika nadharia ya upole, ambayo ilitekeleza jukumu la kuokoa nyuso za maarusi kutokana na matusi yaliyoangaziwa katika nyimbo hizi. Kazi hii ilimsaidia mtafiti kuona jinsi ya kutambua maudhui katika nyimbo za msondo kwani nyimbo hizi haziimbwi kwa lugha ya moja kwa moja na tumepata kujua ujumbe fiche ambao hautolewi kwa maelezo ya moja kwa moja. Ujumbe huwa umefichika kwa kiasi kikubwa sana na husemekana kuwa na matusi kwa kiwango fulani. Hata hivyo utafiti wake ni tofauti na wetu kwani tulichanganua nyimbo za msondo katika jamii ya Wadigo.

Ngome (2014), ambaye alifanya utafiti aliangazia uchambuzi linganishi wa maudhui na majukumu ya nyimbo za harusi za kawaida za jamii ya Wadigo na Waswahili. Kazi hii ilimfaa mtafiti sana kwani alilinganisha nyimbo hizo za harusi za Wadigo alizoziainisha mtafiti huyu na nyimbo za msondo za Wadigo tulizozichambua na kuona kwamba nyimbo hizi ni tofauti kabisa tukizingatia wahusika, wakati na taratibu za nyimbo hizi. Kazi yake ilihusu sana utaratibu wa harusi ya jamii ya Wadigo na kuangazia majukumu na maudhui ya nyimbo hizi za harusi na hakugusia swala la nyimbo za msondo zinazopatikana katika jamii hii.

King’ei (1992), ambaye alichunguza nafasi za nyimbo za taarabu nchini Kenya katika miaka 1963-1990. Alibainisha chanzo, maendeleo na msambao wa nyimbo hizo. Kazi hii, japo ilizungumzia kuhusu maswala mengi, ilimsaidia mtafiti kuangalia maudhui na misamiati iliyotumika katika nyimbo za taarab na pia kugundua kwamba kuna tofauti kati ya nyimbo hizi za taarab na za msondo tukiangazia mtindo wake. Nyimbo za taarab huwa na beti nyingi ilhali nyimbo za msondo huwa na beti moja au mishororo kadhaa.

Kobia (2011), alitafiti majukumu, itikadi na mahusiano ya kiuana katika jamii ya Waigambe, kazi hii ilimsaidia mtafiti kuangalia itikadi zinazotumiwa katika jamii ya Wadigo tukizingatia nyimbo za msondo, kwani sio kila harusi iliyofanyika tulipata nyimbo za msondo. Ni baadhi tu kwani watu wengine katika jamii hawazingatii itikadi hii ya kuwa na nyimbo za msondo. Ijapokuwa kazi yake ilizingatia majukumu, itikadi na mahusiano ya kiuana katika jamii ya Waigambe ilimsaidia mtafiti kuangazia majukumu ya nyimbo hizi za msondo.

Yego (2011), alichunguza nafasi ya mwanamke jinsi inavyotetewa katika nyimbo za taarab Zanzibar na aliangazia nafasi ya mwanamke katika ndoa na majukumu ya mwanamke. Kazi hii ilimsaidia mtafiti kwani aliweza kuchunguza jinsi nafasi ya mwanamke inavyojitokeza katika nyimbo za msondo na kuainisha majukumu ya mwanamke katika ndoa kwani nyimbo hizi huzungumzia maswala ya wanawake pekee. Mtafiti aligundua kwamba katika nyimbo hizi za taarab na msondo ni mwanamke ambaye amepewa majukumu mengi katika jamii kama vile kumridhisha mume na kutunza familia yake.

Mohamed (2015), alichunguza dhima ya nyimbo za ngoma ya msondo wa Pemba ambapo alifafanua kwamba kuna msondo wa wanawake na wanaume na vilevile msondo wa Pemba hupigwa ndani au nje. Vilevile alieleza dhima na majukumu ya nyimbo hizi kama vile kuheshimu na kumuenzi mume, kuwathamini wakuu, kuacha tabia mbaya na kueleza kuhusu maswala ya ndoa. Kazi yake ilimfanya mtafiti kuangazia iwapo nyimbo hizi za

msondo wa Kipemba na msondo wa jamii ya Kidigo unamfanano au unatofautiana kwa kiwango gani. Utafiti huu uligundua kwamba msondo wa Pemba unafanana na msondo wa kidigo tukizingatia maudhui yaliyojitokeza lakini unatofautiana tukizingatia nyimbo zinazoimbwa na utaratibu wa nyimbo hizi kwa mfano kanuni ya mavazi na utaratibu wa nyimbo hizi.

Silau (2013), alichunguza dhima ya nyimbo za Kikaguru katika kukuza na kuimarisha malezi katika jamii ya Kikaguru na kutueleza kwamba nyimbo hizi zinaitwa ‘ndaku’ na zinahusishwa na unyago na jando. Nyimbo hizo hufunza vijana maadili mema na huwa zinafungamana na lugha ya mafumbo na pia hueleza mila na desturi ya jamii hiyo. Kazi hii ilimsaidia mtafiti kwa kuzingatia umuhimu wa nyimbo za msondo katika jamii na kugundua kwamba nyimbo hizi pia zinakuza malezi ya wanawali haswa tukizingatia maswala ya ndoa katika jamii hii ya Wadigo.

Rashid (2013), alichunguza mafunzo ya nyimbo za jando na unyago kwa jamii ya Wahiyao wa Masasi, Tarafa ya Lulindi na anaeleza ya kwamba nyimbo hizi zinaitwa chiputu zinazohusishwa na unyago na lupanda zinazohusishwa na jando. Nyimbo hizi za Wahiyao zinaimbwa na kuchezwa wakati vijana wamebaleghe na hufunza maadili mema katika jamii kama vile utamaduni, uwajibikaji, usafi na masuala ya ndoa. Kazi yake ilimsaidia mtafiti kuangalia uhusiano wa nyimbo hizi za jamii ya Wahiyao na jamii ya Wadigo. Hii ni kwa sababu nyimbo za msondo tunaweza kuzihusisha na nyimbo za unyago katika jamii hii ya Wadigo tofauti ni kwamba nyimbo za Wahiyao huchezwa wakati vijana wamebaleghe ilhali nyimbo za msondo huchezwa wakati wa harusi.

Sayfa (2007), alichunguza athari za nyimbo za harusi kwa mke na mume na kuelezea kwamba nyimbo hizi huwa na athari mbalimbali katika jamii kama vile kuhamasisha wanajamii kuhusu majukumu yao katika ndoa na kulinda miiko ya ndoa. Alieleza kwamba athari nyingi hasi zinazotokana na nyimbo za harusi ni kwa sababu wanajamii hawazingatii

mafundisho yake na miiko yake. Kazi hii ilimsaidia mtafiti kuangalia athari mbalimbali zilizojitokeza katika nyimbo za msondo hata hivyo kazi yake ilitofautiana na yetu kwani tuliangazia maudhui, miiko na athari za nyimbo za msondo na wala sio nyimbo za harusi za kawaida.

Waziri (2016), alichunguza dhima za nyimbo za singo katika kijiji cha Uzini Zanzibar na kueleza kuwa nyimbo hizi huimbiwa bi. harusi siku moja kabla ya kufunga ndoa wakati wa magharibi au usiku. Nyimbo hizi huimbwa huku bi. harusi akisingwa kwa kutumia mafuta ya nazi, liwa na karafuu huku akielezwa majukumu na maadili anayotakikana kufuata katika ndoa. Utafiti huu ulimsaidia mtafiti kuelewa maudhui ya nyimbo za msondo kwani yanashabihiana na maudhui ya nyimbo za singo kama vile kueleza kuhusu umuhimu wa ndoa, maadili katika ndoa, kufanikisha tendo la ndoa na mengine mengi. Hata hivyo utafiti huu ulitofautiana kwani tulichanganua maudhui, miiko na athari za nyimbo za msondo katika jamii ya Wadigo.

Makange (2015), alilinganisha fani za kiutendi katika nyimbo za harusi miongoni mwa jamii ya Wataveta na Waswahili na kueleza kwanza kuhusu utaratibu wa harusi wa jamii hizi mbili. Alieleza kwamba katika jamii hizi kuna mafunzo wanayopewa wasichana wanapovunja ungo na kwamba katika jamii ya Wataveta mafunzo haya hufunzwa katika sehemu iitwayo ngondi na jamii ya waswahili mafunzo hayo hupewa na makugwi. Mafunzo haya kwa jumla huhusu jinsi ya kuishi na kumtunza mume. Utafiti huu ulitusaidia kuangazia maudhui ya nyimbo za msondo hata hivyo utafiti huu ulitofautiana kwani hatukushughulikia fani katika nyimbo za msondo.

2.3 Msingi wa Nadharia

Katika utafiti huu, mtafiti alitumia nadharia ya uhalisia. Nadharia hii ilianza kutumika katika fasihi kule ufaransa katikati ya karne ya kumi na tisa na baadaye nadharia hii ilisambaa kule Uingereza, Urusi na Marekani.

Hegel (1975, 1979) alilitumia neno uhalisia kumaanisha kazi ya sanaa iliyo na wahusika ambao matendo yao yanachochewa na hali ya kisaikolojia iliyowazunguka. Uhalisia unahusu uigizaji wa mazingira anamopatikana mwanadamu. Kulingana na Walder (1995), alieleza kwamba, uhalisia ni kuandika kazi ya kubuni inayotokana na kutazama ulimwengu wa kawaida wa wanaume na wanawake katika jamii kwa kutumia lugha inayoeleweka kwa hadhira pana.

Nadharia hii hutumia usimulizi wa kimuhakati. Huu ni usimulizi ambao unasimulia matukio kama yanavyotokea katika ulimwengu halisi au kwa namna inayokaribiana sana na hali iliyoko katika jamii. Uhalisia husisitiza uwasilishaji wa maisha ya kijamii kwa uamilifu na usahihi mkubwa. Mtazamo huu unatia mkazo kwenye uwasilishi wa mambo ambayo yanaonekana katika jamii.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), uhalisia husisitiza uwasilishaji wa maisha ya jamii kwa uamilifu na usahihi mkubwa, mtazamo huu unaweka mkazo kwenye uwasilishi wa mambo ambayo yanaonekana katika jamii. Waandishi wanaoandika kwa msingi huu wanatarajiwa kuyaakisi maisha ya kijamii katika ngazi za kijamii, kiuchumi, kitamaduni au kisiasa, kutoa picha za wahusika, matukio na mandhari ambayo yanaoana kwa kiasi kikubwa na uhalisi wa jamii.

Uwasilishaji wa maisha katika kazi za kihalisia ni dhana ya ushabihikweli. Msisitizo mkubwa wapatikana kwenye juhudi za kuukaribia ukweli uliopo katika jamii inayohusika. Kwa mtazamo huu, kazi nyingi zinaishia kuyakwepa matukio au mandhari yasiokuwa ya kawaida. Waandishi wa kihalisia huchukulia kuwa picha zinazopatikana kwenye kazi zao pamoja na yaliyomo huwiana na ukweli wa jamii zinazohusika.

Kwa mujibu wa Ntarangwi (2004), nadharia hii ya uhalisia katika upana wake humaanisha uwakilishaji wa uhalisia wa mambo katika fasihi. Nadharia hii ilizuka katika karne ya kumi na tisa hususan kwa lengo la kupinga mkondo wa ulimbwende. Mhalisia huamini katika

matokeo ya mambo ya ukweli unaoangazia ni ule unaoweza kuonekana na kuthibitisha kwa tajiriba.

Vilevile, wanauhalisia huiamini demokrasia kama hali ya maisha na malighafi ya kuelezea maisha ya kawaida, ya kadiri na ya kila siku. Hivyo basi, uhalisia hujikita katika mambo yaliyopo, tukio makhsusi na matokeo yanayoweza kuthibitika. Imani ya mhalisia ni kwamba kazi ya fasihi inapaswa kuwaweka wanajamii husika katika ulimwengu wao wa kawaida wa kweli na halisi. Kwa hivyo, hata picha za ulimwengu atakazoumba msanii zinapaswa kudhihirisha hali hiyo.

Njogu na Wafula (2007), wanasema nadharia hii ya uhalisia ndiyo muhimu zaidi kutokea katika karne ya kumi na tisa na ishirini na pengine itaendelea kutuathiri kwani inaashiria uwezo wa kusawiri au kueleza hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakiki wa maisha.

Nadharia hii inapendekeza kazi ya fasihi iwasilishe maisha ya jamii katika mazingira yake ya kawaida. Katika hali hii tulihusisha nadharia hii ya uhalisia na uchanganuzi wa nyimbo hizi za msondo kwani nyimbo hizi zinachezwa katika mazingira halisi na zilionyesha mtazamo halisi wa jamii hii kuhusiana na mila na utamaduni wao katika maswala ya ndoa ambayo ni muhimu sana katika maisha ya binadamu.

2.3.1 Mihimili ya Nadharia ya Uhalisia katika Uchanganuzi wa Nyimbo za Msondo

Nadharia hii ina mihimili mitano ambayo ilitumika kukamilisha utafiti huu.

1. Nadharia hii inashikilia kwamba hali zote za maisha ya kijamii huelezwa katika uhalisi wake kama unavyoonekana wala sivyo unavyofikiriwa kuwa. Mtafti alitumia mhimili huu kuonyesha uhalisia wa nyimbo hizi za msondo kwa kutoa thibithisho kwamba zinapatikana katika jamii na pia kuziorodhesha baadhi ya nyimbo hizi na kuzieleza maana yake.

2. Uhalisia unaangazia hali ya wahusika na lugha wanayotumia ambayo msomaji anakumbana nayo katika maisha yake ya kila siku. Mtafiti alitumia mhimili huu kuchambua lugha inavyotumika katika nyimbo za msondo. Lugha hii inayotumika katika nyimbo hizi hutumika katika maisha ya kila siku hususan katika maisha ya ndoa ijapokuwa lugha hii ilijaa mafumbo mengi. Tukizingatia wahusika walioshiriki katika nyimbo hizi tuliwaona ni wahusika wa kawaida waliotambulika na wanajamii.

3. Nadharia hii inachambua kazi ya sanaa kama zao linalojitosheleza. Mhimili huu ulitumiwa na mtafiti kuchambua nyimbo za msondo na kuona kwamba matukio yaliyotokea wakati wa kuimba na kucheza nyimbo hizi hukamilisha malengo ya nyimbo hizi na maudhui yaliyokusudiwa kupitishwa na wanajamii kama vile kuna nyimbo zinazohusu uke wenza, kupeana vijembe na kupeana tahadhari katika jamii.

4. Uhalisia huangazia vielelezo vya kihistoria vinavyosababisha mabadiliko katika jamii. Hali hii inamaanisha kwamba uhalisia unaweza kubadilika kufuatia mabadiliko ya hali mbalimbali za kijamii. Mtafiti alitumia mhimili huu kudhihirisha kwamba nyimbo hizi za msondo katika jamii ya Wadigo zilipitia mabadiliko fulani. Kwa mfano hapo kale katika jamii ya Wadigo, walipeleka wasichana wao kwa makungwi kukaa huku wakifundishwa mambo ya unyumba kwa takriban mwezi mmoja. Lakini kwa sababu ya mabadiliko kadha wa kadha katika jamii kama vile watu kuhamia mijini, hali ya kiuchumi na masuala ya kidini mambo haya yalipotea na kuachwa na nyimbo za msondo ndizo huimbiwa bi. harusi na kufundishwa mambo ya unyumba wakati wa sherehe ya harusi.

5. Nadharia ya uhalisia inaelezea kwamba fasihi lazima izingatie matukio na mandhari ya kawaida yanayoweza kupatikana katika jamii. Wamitila (2002), anasema kwamba fasihi ni kioo cha jamii. Mhimili huu ulitumiwa na mtafiti kueleza nyimbo hizi zilitumiwa kama kioo cha jamii kwa namna ambavyo hutoa picha ya binadamu katika mazingira yake. Nyimbo hizi za msondo huangazia mambo kadha wa kadha katika jamii. Mambo yaliyoakisiwa

yalihusu unyumba kwa hivyo mhimili huu wa kuiona fasihi kama kioo cha jamii, ulionyesha jinsi jamii ya Wadigo walivyothamini maisha ya ndoa kama kiendelezo cha jamii na kupeana mafunzo kuhusiana na masuala haya ya ndoa.

Mtafiti alizingatia nadharia ya uhalisia katika kipengele cha uchambuzi wa data na kuangalia ukweli uliopatikana na kuuwasilisha ulivyo bila kupunguza wala kuongeza ukweli uliopatikana katika matokeo ya utafiti huu.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea mbinu za utafiti kwa kuzingatia vigezo kama vile utaratibu wa utafiti, maelezo ya kijiografia, jumuiya ya uteuzi wa sampuli na mbinu za kukusanya data. Vilevile inaelezea jinsi data ilivyochanganuliwa na kuwasilishwa ili kufikia malengo ya utafiti.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika eneo la Likoni mitaa ya Jamvi la wageni na Migombani. Mtafiti aliteuwa mitaa hii kwa sababu ni rahisi kuifikia kwani inapatikana baada ya kivuko cha feri. Mitaa hii pia huwa kuna sherehe nyingi za harusi ambapo nyimbo za msondo huimbwa kwa hivyo data iliyopatikana ni ya kutosha kuyafikia malengo ya utafiti huu.

3.3 Mbinu za Utafiti

Mtafiti alitumia mbinu ya maktabani na mtandao kusoma tasnifu kuhusu nyimbo tofauti na maelezo kuhusu nadharia ya uhalisia iliyotumika katika utafiti huu. Vilevile Mtafiti alikwenda nyanjani na kufanya uchunguzi shirikishi katika sherehe za harusi ambapo nyimbo za msondo ziliimbwa na kuchezwa. Hali hii ilimuwezesha mtafiti kujua namna sherehe hizi zilivyoendeshwa na pia alisikiza nyimbo zilizoimbwa. Baada ya kufanya uchunguzi shirikishi katika sherehe hizi mtafiti aliweza kuonana na baadhi ya makungwi waliokuwa katika sherehe ya msondo na pia baadhi ya wanawake waliohudhuria katika sherehe ya harusi. Mtafiti alichagua watu 50 ambao walipatikana kwani mmoja baada ya mwingine waliweza kumueleza mtafiti kuhusu mtafitiwa mwingine ambaye aliweza kutusaidia kukusanya data ya utafiti huu.

Mtafiti alikuwa katika mazingira mazuri ya kuuliza maswali kulingana na yale aliyoyaona wakati alifanya uchunguzi shirikishi. Mtafiti vilevile aliwahoji watu ambao hawashiriki moja kwa moja katika sherehe hizi za msondo lakini wanafahamu kwamba kuna masuala

haya yanayotokea katika jamii. Kwa hivyo mtafiti aliwahoji wanaume katika ndoa na wanawake katika ndoa ambao hawakuchezewa nyimbo za msondo.

3.4 Uteuzi wa Sampuli

Utafiti huu ulitumia uteuzi wa kimaksudi kwani mtafiti aliwataka watu wanaohusiana moja kwa moja na nyimbo za ngoma hizi za msondo. Sampuli ya watu hawa walichaguliwa kimaksudi kwani ni watu waliojuana wao kwa wao na ukipata wachache wao waliweza kupeana majina ya wenzao ambao walishirikiana katika kuimba na kucheza nyimbo hizi za msondo.

Jumuiya ya utafiti huu ulijumlisha makundi manne ya watu wakiwemo makungwi ambao hupiga ngoma hizo, huimba na kupeana mafunzo kwa bi. harusi katika sherehe hii. Wanawake waliomo katika ndoa ambao walichezewa na kuimbiwa nyimbo za msondo, ili watufahamishe manufaa waliyoyapata walipochezewa nyimbo hizi za msondo. Wanawake katika ndoa ambao hawakuimbiwa na kuchezewa nyimbo za msondo, watufahamishe kama wanafahamu kuwa kuna nyimbo hizi za msondo na iwapo wanafahamu maudhui, miiko na athari za nyimbo hizi katika jamii. Vilevile watufahamishe iwapo wanadhani wangetekeleza majukumu yao ya ndoa ipasavyo iwapo wangeimbiwa na kupewa mafunzo ya nyimbo za msondo. Mwishowe wanaume katika ndoa ili kupata hisia zao kuhusu nyimbo hizi za msondo.

Kwa hivyo, jumuiya ya watafitiwa ni 50 wakiwemo makungwi 10, wanandoa wanawake 15 waliochezewa nyimbo za msondo. Wanawake 15 ambao hawakuchezewa nyimbo hizi na wanaume 10 walioko katika ndoa. Mtafiti alitaka kujua iwapo wanaume wanafahamu mambo haya kuwa yanatendeka na maoni yao ni yapi kuhusu nyimbo hizi za msondo. Mtafiti vilevile aliweza kupata jumla ya watafitiwa wote hamsini waliohitajika katika utafiti huu.

Mtafiti alizingatia umri wa makungwi usiopungua miaka arubaini na tano kwa sababu makungwi waliobobea katika kazi hii huwa ni watu wakutimu miaka hii na zaidi. Watafitiwa waliosalia walikuwa kati ya miaka ishirini na nane hadi arubaini kwa sababu mtafiti na msaidizi wake wako katika umri huu na ilikuwa rahisi kupata taarifa kutoka kwa watafitiwa. Vilevile watafitiwa wa umri huu ni mwafaka zaidi kwani iwapo waliimbiwa nyimbo za msondo na kupewa mafundo yake basi walikuwa katika nafasi nzuri kukumbuka mambo haya kwani hawajakaa muda mrefu katika ndoa zao.

Watafitiwa hawa walipatikana wote lakini kati yao kuna wale hawakuweza kujibu maswali yote ya utafiti. Hii ni kwa sababu ya ukosefu wa elimu ya kufafanua maswala mengine yanayohusiana na nyimbo za msondo. Hali hii ilifanya mtafiti kuwahoji watafitiwa wengine ambao angalau walikuwa na welewa zaidi kuhusiana na nyimbo hizi za msondo ili kuwafidia wale ambao hawakuweza kujieleza kwa kina.

Vilevile mtafiti alizingatia hali yao ya ndoa kwamba lazima wangekuwa katika ndoa isipokuwa baadhi ya makungwi kwa sababu wengi wao ni watu wazima. Makungwi hawa baadhi yao walikuwa katika ndoa maishani na kwa wakati wa kufanyika utafiti huu hawakuwa katika ndoa kwa sababu kadha wa kadha kama vile kutalikiana na mume au ujane.

3.5 Mbinu za Kukusanya Data

Mtafiti alifanya uchunguzi shirikishi ambapo ni hali ya kushuhudia matukio yanavyotendeka na kukusanya taarifa. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kukusanya taarifa kwa mpangilio mzuri, kutaamali matendo na matukio ya kijamii moja kwa moja yalipotokea katika mazingira yake asilia. Mtafiti alihudhuria harusi ambazo nyimbo hizi ziliimbwa na kuchezwa na kuona matendo mbalimbali yaliyotendeka na kuweza kukusanya data kuhusu nyimbo hizi za msondo.

Mtafiti pia alitumia mwongozo wa mahojiano ambayo ni maswali tofauti yaliyomuwezesha mtafiti kupata habari zaidi iliyohitajika katika utafiti huu. Mahojiano haya pia yalimuwezesha mtafiti kupata maelezo zaidi kutoka kwa watafitiwa ambayo hayakuwa katika maswali yaliyoratibiwa katika mwongozo huo wa mahojiano. Mahojiano haya yalichukua takriban dakika ishirini hadi thelathini kwa kila mtafitiwa. Watafitiwa wote 50 walipatikana na kujibu maswali hayo ijapokuwa baadhi ya watafitiwa hawakuweza kujibu maswali yote kwa sababu hawakuwa na uzoefu wa masuala haya ya msondo. Vilevile watafitiwa hawa walikataa kurekodiwa kutumia kinasa sauti na walipendelea mtafiti kuandika tu yale waliyoyasema.

3.6 Mbinu za Uchanganuzi wa Data

Nyimbo za kitamaduni za Kiafrika mara nyingi huchukuliwa kama sanaa ya kufikirika ilhali nyimbo hizi huzingatia matumizi yake. Utumiaji wa muziki husemekana kuwa haujajitosheleza ikiwa wachanganuzi watatupilia mbali maswala ya kijamii katika miziki hii. Kwa hiyo wachanganuzi wa nyimbo za kitamaduni ambazo hujumlisha nyimbo zote za Kiafrika lazima wazingatie shughuli mahususi ambayo muziki fulani imejikita (Agawu 2001).

Utafiti huu ulikuwa wa kithamano uliochunguza mambo katika mandhari yake halisi ili kubaini au kufasiri matukio kulingana na mtazamo wa watu. Data iliyochanganuliwa na mtafiti ilihusu maudhui ya nyimbo za msondo na athari zake kwa wanandoa katika jamii ya Wadigo. Kulingana na uhalisia wa data hii, ilimbidi mtafiti ashuhudie matukio mbalimbali ya nyimbo hizi za msondo.

Nyimbo zilizopatikana ni nyingi lakini mtafiti aliweza kuzijumlisha katika makundi tofauti kulingana na maudhui yanayojitokeza katika nyimbo hizo. Mtafiti alichagua nyimbo kumi na nane zilizomuwezesha kupata masuala tofauti na baadaye alizichanganua. Vilevile mtafiti alichanganua maelezo yote aliyoyapata kutoka nyanjani na kuyaeleza ipasavyo na mwishowe kupata matokeo ya utafiti huu.

3.7 Uwasilishaji wa Data

Mtafiti alitumia grafu ili kuchanganua data hii iliyohusu maudhui ya nyimbo za msondo na athari zake kwa wanandoa katika jamii ya Wadigo na kuonyesha asilimia zilizopatikana kutoka kwa watafitiwa. Asilimia hizi zilitumika kueleza msimamo wa idadi ya watafitiwa kuhusiana na malengo yetu ya utafiti na kueleza mtazamo wao kuhusiana na nyimbo hizi za msondo. Mtafiti aliorodhesha nyimbo zote alizozipata kisha akazitafsiri na kueleza maudhui yaliyojitokeza katika nyimbo hizo. Vilevile mtafiti aliwahoji watafitiwa kuhusu maudhui, miiko na athari za nyimbo hizi za msondo. Watafitiwa wengi waliweza kuelezea maudhui ya nyimbo hizi bila ya wao kutambua aina za nyimbo hizi. Vilevile watafitiwa waliweza kutaja baadhi ya miiko inayohushishwa na nyimbo hizi za msondo. Watafitiwa waliweza kutoa athari za nyimbo hizi na mafundisho yake kwa kuelezea tabia na matendo ya wanajamii walioimbiwa nyimbo za msondo wakati wa harusi zao. Mtafiti alitumia maelezo aliyoyapata kuonyesha nyimbo hizi zinabeba maudhui yanayohusu unyumba na yasiyohusu unyumba. Mtafiti aligundua wanajamii wengine wanafahamu miiko hii wengine wanafahamu baadhi tu na wengine hawafahamu kabisa miiko hii. Mtafiti vile vile alichanganua athari zilizojitokeza kupitia kwa maswali ya mahojiano na kubaini kwamba kuna athari chanya na hasi zilizohusishwa na nyimbo hizi za msondo na mafundisho yake.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Katika uwasilishaji na uchanganuzi wa data, mtafiti alizingatia malengo ya utafiti huu yakiwemo maudhui ya nyimbo za msondo, miiko iliyofungamanishwa na nyimbo hizi na athari zilizohusishwa na nyimbo za msondo katika jamii ya Wadigo. Uchanganuzi huu uliwasilishwa kutumia grafu na pia kimaelezo kwani mtafiti alieleza kwa kina juu ya data iliyokusanywa.

4.2 Uchambuzi wa Maudhui ya Nyimbo za Msondo

Nyimbo za msondo hubeba maudhui kadha wa kadha kulingana na maneno yanayotumika katika wimbo fulani, nyimbo zilizokusanywa ni kumi na nane, hii ni kwa sababu mtafiti alipata nyimbo kadhaa tofauti ambazo zinazungumzia maudhui sawa.

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999), maudhui ni ujumbe wa jumla kuhusu matukio, kitu, wahusika au hali ya maisha kama yanavyojitokeza katika kazi ya fasihi. Kulingana na Wamitila (2003) maudhui ni yaliyomo au jumla ya masuala yanayozungumziwa katika kazi ya kifasihi. Katika nyimbo hizi za msondo mtafiti aliangalia maudhui yaliyojitokeza katika nyimbo hizi na kueleza ni mambo gani yaliyozungumziwa zaidi katika nyimbo hizi za msondo kuliko mengine hususan tukizingatia hali ya maisha katika jamii hii.

Watafitiwa waliohojiwa walikiri kwamba nyimbo za msondo zilibeba maudhui yaliyohusiana na unyumba na vilevile maudhui yasiyohusiana na unyumba. Mtafiti aliweza kuyafikia maudhui haya kwa kuzichanganua nyimbo hizi za msondo na kupata matokeo ya utafiti huu.

Kielelezo cha 1: Maudhui yanayohusishwa na Nyimbo za Msondo



Utafiti huu uligundua kwamba asilimia thamanini ya makungwi wanakiri kwamba nyimbo za msondo zina maudhui yaliyohusu unyumba ilhali asilimia ishirini wanasema kwamba mbali na maudhui ya unyumba kuna maudhui mengine yasiyohusiana na unyumba ambayo yalipatikana katika nyimbo hizi za msondo.

Asilimia sabiini ya wanawake waliochezewa nyimbo za msondo wanakiri kwamba nyimbo hizi zina maudhui ya unyumba ilhali asilimia thelathini wanakiri kwamba maudhui mengine mbali na ya unyumba pia yalipatikana katika nyimbo hizi.

Asilimia sitini ya wanawake katika ndoa ambao hawakuchezewa nyimbo za msondo walikubali kwamba maudhui ya nyimbo hizi yalihusu unyumba. Asilimia arubaini kati yao wanakiri kwamba kuna maudhui yasiyohusiana na unyumba ambayo pia hupatikana katika nyimbo hizi.

Asilimia sitini ya wanaume katika ndoa wanakiri kwamba nyimbo hizi za msondo zina maudhui yaliyohusiana na unyumba ilhali asilimia arubaini walisema kwamba mbali na unyumba kuna maudhui yasiyohusiana na unyumba.

Kutokana na data iliyokusanywa na mtafiti, iliashiria kwamba jamii ya Wadigo walikubaliana kwamba nyimbo za msondo zina maudhui yaliyohusiana na unyumba ambayo yanafaa kufunzwa. Jamii inafaa kuhamasishwa jinsi ya kutumia maudhui haya kwa manufaa yao na wasiende kinyume na mafundisho haya. Mtafiti aliweza kukusanya nyimbo tofauti zilizothibitisha kwamba kuna maudhui yaliyohusu unyumba na vilevile maudhui yasiyohusu unyumba yaliojitokeza katika nyimbo za msondo.

4.3 Uchambuzi wa Maudhui ya Nyimbo za Msondo yanayohusu Unyumba

Mtafiti aliweza kukusanya nyimbo kadha wa kadha zinazoelezea kuhusu maswala ya unyumba. Nyimbo hizi zilipatikana kupitia mahojiano na makungwi ambao walimuimbia mtafiti nyimbo hizi walizitafsiri kwa lugha rahisi na kuzieleza maana zake.

Watafitiwa wengine kama vile wanawake ambao hawakuchezewa nyimbo hizi za msondo na watafitiwa wanaume walikiri kwamba nyimbo hizi za msondo zina maudhui ya unyumba lakini hawakuweza kutoa ushahidi wa nyimbo yoyote wanayoifahamu iliyoeleza maudhui hayo. Walikubaliana na maudhui haya kwa sababu nyimbo hizi huimbwa wakati wa harusi na kwamba lazima zingezungumzia mambo ya unyumba.

Nyimbo hizi zilitumia lugha ya kimafumbo ilikuficha ukali wa maneno halisi iwapo yangetumika kuimbia nyimbo hizi.

4.3.1 Kuonyesha Nafasi ya Ndoa katika Jamii

Wimbo wa 1

Baba niundie chombo nisafiri niende amu

Nikamtwae mwengereza na nduguye mkadamu

Kama si kuvunja ngome niite mwanaharamu x3

Baba nitengezee chombo nisafiri niende Lamu

Nikamchukue Mwengereza na ndugu yake mkadamu

Kama si kuvunja ngome niite mwanaharamu x3

Wimbo huu ulileta dhana kwamba, mwari amwambia baba yake yuko tayari kwa safari ya ndoa kwa yeyote atakayejaliwa naye kwa sababu yeye ni msichana aliyejilinda na anataka kuanza maisha ya ndoa kihalali kwani yeye si mwanaharamu na hataki kupata mwanaharamu kwa kushiriki maswala ya ngono kiholela kabla ya ndoa.

Wimbo huu huimbwa kuhamasisha jamii kwamba mwari akifika wakati wa kuolewa, ni jukumu la wazazi kumtafutia mtoto wao mchumba ili aepukane na kuwatia wazazi aibu. Kwa mfano, mwari anaweza pachikwa mimba akiwa nyumbani.

Wimbo huu ulionyesha kwamba jamii ya Wadigo wanathamini ndoa katika jamii kama njia ya kuendeleza vizazi vijavyo na kuhimiza vijana katika jamii hii kuoa au kuolewa.

4.3.2. Kuonyesha Umuhimu wa Tendo la Ndoa

Mtafiti alipata nyimbo zenye maudhui yanayohusiana na tendo la ndoa, vilevile mtafiti aligundua kwamba nyimbo nyingi za msondo zinazungumzia masuala ya ngono. Katika hali hii mwari huelezewa kuhusiana na tendo hilo kupitia kwa nyimbo kadha wa kadha ambazo huchezwa na kuonyeshwa mizungu tofauti ya kutenda kitendo hicho cha ndoa.

Mwari hufundishwa jinsi ya kuregua na iwapo atashindwa, huchapwa kwa myugwa hadi pale mashangazi zake watakapomkomboa kwa kutolewa pesa. Wakati mwari anaponengua

kiuno huwa amezungukwa na wanachama hao wa msondo huku akipigiwa makofi ili kumpa motisha wa kuendelea kukata kiuno.

Mtafiti aliweza kuchagua nyimbo tatu kati ya nyimbo nyingi ambazo zilikuwa na maudhui haya ya kuonyesha tendo la ndoa.

Wimbo wa 2

Mtaimbo

Mwimbaji : Wateleza huo

Kiitikio : Hauna laika

Mwimbaji : Ni mwembamba huo

Kiitikio : Hauna laika

Mwimbaji : Una tundu huo

Kiitikio : Hauna laika

Mwimbaji : Ukiupeleleza mtaimbo, wateleza mtaimbo

Mtaimbo ni neno la kimafumbo lililotumika kuashiria sehemu ya siri ya mume na kuelezea jinsi mtaimbo ulivyo kwamba ni mwembamba una tundu na huteleza na kwamba mtaimbo huo hauna mfano wake. Wimbo huu huimbwa kutumia mafumbo kueleza kuhusu tendo la ndoa na kueleza jinsi uume unavyokaa, kueleza ile hali ya kujamiiana baina ya mume na mke.

Wimbo wa 3

Gandomfuko

Huko baharini kuna nyama, aitwa Gandomfuko

Ukitaka kula nyama, paka umfate kuko

Wende ukale nyama, gando uliriche kuko

Huko baharini kuna nyama aitwa Gandomfuko

Ukitaka kula nyama, paka umfate huko

Wende ukale nyama, gando uliache huko

Gandomfuko ni neno limetumika kuashiria sehemu ya siri ya mume na kwamba ukitaka kufanya tendo la ndoa lazima umfate huko aliko na ukimaliza *kula nyama*, kumaanisha baada ya kujamiiana, umuweke vizuri na umuache hapo ulipompata.

Wimbo wa 4

Tamu tamu ta tate x2	Tamu tamu ta tate*x2*
Chanda na pete	Chanda na pete
Ulimi na mate	Ulimi na mate
Huo mzungu siumanyire x3	Huo mzungu sikuujua x2

Wimbo huu ulielezea utamu wa tendo la ndoa na kwamba mume na mke wakijamiiana ni kama chanda na pete au ulimi na mate na huzidi utamu iwapo mizungu inayotumiwa kufanya tendo la ndoa ni ya aina tofauti, kumaanisha kwamba lazima mwari atumie mitindo tofauti ya kutekeleza tendo la ndoa.

4.3.3 Kuonyesha Mitindo tofauti ya Ngono

Mtafiti alipata nyimbo zilizoashiria maswala ya ngono na mitindo tofauti inayotumiwa kwa ajili ya kupeana chakula cha ndoa. Nyimbo hizi hufunzwa mwari aina tofauti za kufanya kitendo hicho cha ndoa na kunengua kiuno kwa mitindo hiyo tofauti tofauti. Mtafiti aliweza kukusanya nyimbo zifuatazo.

Wimbo wa 5

Kunguru ndege ayumba yumba	Kunguru ndege ayumba yumba
Nipelekeni kwa somu nikausore mirimo x 2	Nipelekeni kwa somu nikaokote mitindo x 2

Kunguru ndege ilichukua nafasi ya mwari kwamba anayumbayumba anataka apelekwe kwa kungwi akajifunze mizungu inayohusiana na tendo la ndoa .Wimbo huu huimbiwa mwari

na kumfahamisha kuwa bado hajajua mizungu inayohusishwa na tendo la ndoa, kwa hivyo lazima ajiweke tayari kujifunza mizungu hiyo kutoka kwa makungwi wake ndio aweze kuwa mwanamke wakisawasawa.

Wimbo wa 6

Kunguru na mwewe watetea ndege paruanja x2

Kunguru na mwewe watetea ndege uwanjani

Kunguru na mwewe ni maneno yaliyotumika kimafumbo kuashiria mume na mke wakiwa katika tendo la ndoa. Wimbo huu huimbwa wakati ambapo makungwi wanamuonyesha mwari jinsi ya kufanya tendo la ndoa.

Wimbo wa 7

Nafita mzungu wangu mwari sina	Naficha mzungu wangu mwari sina
Ajaliwaye naende akauchole x3	Ajaliwaye aende akauchukue x3

Somu anasema ya kwamba anaficha aliyoyajua kuhusiana na tendo la ndoa kwa sababu hana mwari wa kumfundisha mzungu huo na yule ambaye atajaliwa kuwa na mwari basi anaweza kwenda kuuchukua mzungu huo ili aweze kuutumia.

Wimbo wa 8

Chimba chimba x3	Chimba chimba
Makungwi arore paruwanja	Makungwi waone uwanjani

Chimba chimba kumaanisha kukata kiuno paka chini ili makungwi wakuone uwanjani.

Wimbo huu huimbiwa mwari wakati ambapo ameonyeshwa mzungu fulani na alitakikana kuuiga kwa kucheza huku watu wote wanamuangalia na iwapo mwari atashindwa, basi ataimbiwa nyimbo za kumkashifu kwa kushindwa kukata kiuno.

4.3.4 Nafasi ya Mwanamke katika Ndoa

Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004:300) inasema kuwa, “nafasi ni palipo patupu na ambapo panaweza kuwekwa kitu”. Ufafanuzi huu ukiwekwa katika muktadha wa kijamii una maana kwamba kila mmoja ana mahali pake alipotengewa na jamii ili apate kushiriki katika mambo ya kijamii. Katika jamii ya Wadigo wanawake ni kama pambo la nyumba miongoni mwa majukumu mengine kama kulea**.** Mtafiti alipata wimbo huu unaoelezea nafasi ya mwanamke katika ndoa.

Wimbo wa 9

Nipeni kungu nitafune x 2	Nipeni kungu nitafune
Ni yamezee mate, nijivute	Niyameze mate nijivute
Bembereze mato, kwa waume	Nilegeze macho kwa wanaume

Wimbo huu unamfundisha mwari nafasi yake katika jamii kama mke, kwamba yeye ni pambo la nyumba na lazima kuwa mpambe ili aweze kuwa na mvuto kwa mumewe. Wakati wote, anahitajika kuwa mzuri na mrembo kwa kuhakikisha anakoga vizuri na kujipamba kutumia vipodozi kadha wa kadha kama vile wanja, rangi ya mdomo, mafuta ya kunukia, kujifukiza na udi avae pete, mkufu, bangili, vikuku na kadhalika. Upambe huu unahitajika ili kufanikisha tendo la ndoa.

4.3.5 Uke Wenza katika Jamii

Uke wenza ni hali ambapo wanawake wawili au zaidi wanawekwa na mume mmoja. Mume huyu anaweza kuwa amewaowa wanawake hawa wawili au ameowa mmoja lakini ana uhusiano wa kando na mwanamke mwengine ambaye siye mkewe wa sheria.

Wimbo wa 10

Mke mwenzangu mume ametwawa	Mke mwenzangu mume amechukuliwa
Na atwawee mwana kutwawa x2	Na achukuliwe mwana kuchukuliwa
Na huku endako endee akatwawe x2	Na huko anakokwenda pia akachukuliwe

Na bendera yangu ninayo mwenyewe x2 Na bendera yangu ninayo mwenyewe

Neno bendera limetumika kuashiria uke, wimbo huu unamaanisha ya kwamba hata mume akiibwa na mwanamke mwingine hakuna tatizo lolote kwani jambo la muhimu ni kwamba mwanamke bado amebaki na uke wake na ndicho kitu muhimu katika tendo la ndoa.

Wimbo huu ulieleza maudhui ya unyumba kwamba katika jamii hii ya Wadigo, wanaume wanaruhusiwa kuwa na wake zaidi ya mmoja. Wanawake walielezwa ya kwamba ni jambo la kawaida kwa mume kuwa na wake zaidi ya mmoja na iwapo haya yatatokea katika ndoa, basi wanastahili kuwa wavumilivu na kukubali hali hii, kwa sababu dini na tamaduni inaruhusu mume kuoa wake zaidi ya mmoja.

4.3.6 Kupeana Vijembe

Kulingana na Ngome (2012), vijembe ni hali ya wanawake kurushiana maneno ambayo yamejaa matusi, kejeli na bezo wakiwa na nia ya kuudhiana. Mara nyingi hali hii hutokea pale wanawake wamepopokonyana mabwana. Wakati mwingi huwa baina ya mwanamke muhuni na aliyeolewa. Mtafiti alipata wimbo ufuatao.

Wimbo wa 11

Mwimbaji *Aliniahidi huyo kishindo, ataniondoa mimi mgandamo*

Lakini silaha sijaiona, mgandamo sijaiona

Sijali mama……

Kiitikio *Sijali*

Mwimbaji *Sijali maneno*

Kiitikio *Sijali*

Mwimbaji *Sijali kusengenywa*

Kiitikio *Sijali*

Kishindo ni neno limetumika kuashiria mwanamke anayetembea na mume wa mwenzake ilhali mgandamo ni mwanamke aliyemthibiti mumewe na kwamba amemshikilia vizuri kimapenzi na hakuna mtu yeyote anayeweza kumpokonya kwa sababu silaha zote za mapenzi amezihimili vilivyo.

Nyimbo hii ina maudhui ya unyumba ambapo huwasuta wanawake walioko katika uke wenza. Wimbo huu humfundisha mwari kuwa mwanamke ni kujiamini na ikiwa mwanamke atatumia silaha zote za mapenzi atakazofundishwa na kungwi wake basi hakuna mwanamke yeyote atakayeweza kumpokonya mumewe na wataishi miaka mingi ya maelewano na mapenzi tele bila kugombana kwa mara kwa mara.

Vile vile, wimbo huu una maudhui ya kuwaasa wanawake katika ndoa kwamba ni kawaida kwa mwanamume kuwa na hawara nje. Si jambo geni katika ndoa kwa hivyo anastahili avumilie. Uhusiano huo na hawara utaisha na yeye mke anastahili aongeze mapenzi zaidi kwa mumewe ndipo mume huyo azinduke na kuachana na hawara huyo.

4.3.7 Kusifu na Kukashifu Matendo

Mtafiti alipata wimbo huu unaoleta dhana ya kusifu matendo mazuri katika jamii.

Wimbo wa 12

Nipani kiribiti eeeh	Nipeni kiribiti
Nng'arire mwari	Nimng'arie mwari
Nng'a nnga' nga'rare	Nimng'arie ng'arie mwari
Mwari ng'are ng'are x3	Mwari ng'are nga're

Wimbo huu, makungwi humsifu mwari kwa kutangaza kwamba watu waje wamuone wasoona vizuri wapewe kiribiti kwani mwari anajua mizungu na yuko tayari kwa tendo la ndoa.

Vilevile mtafiti alipata nyimbo zinazokashifu matendo fulani katika jamii.

Wimbo 13

Eeeeh mwari ashindwa na mzungu x 3

Wimbo huu huimbwa wakati ambapo mwari alishindwa kukata kiuno ili kuiga mzungu alioonyeshwa na makungwi wake. Mwari aliimbiwa wimbo huu hadi pale mwari atakombolewa na kungwi wake mkuu kwa kutoa ada fulani ili mwari apewe mzungu mwingine atakaoweza kuutegua kwa kufunzwa jinsi ya kukata kiuno.

4.3.8 Utunzaji wa Siri katika Ndoa

Kulingana na Rashid (2013), elimu ya nyimbo za jando na unyago inahitaji siri kubwa kwa anayeipata. Na ili iwe siri, anayepewa ni lazima awe amepevuka kiakili na kimwili. Kutokana na maoni haya mtafiti amegundua kwamba kuna nyimbo za msondo vilevile zinazozungumzia kuhusu utunzaji wa siri katika ndoa.

Wimbo wa 14

Usinende nisema x3 Mwari

*Usinende nisema kama somu ana marewerewe ya matako. (*kiitikio*)*

Usiende kunisema mwari x3

Usiende kunisema kama somu ana marewerewe ya matako. (kiitikio)

Wimbo huu humfunza mwari kuwa msiri kwamba lolote atakalofundishwa na somu yake asiende kulisema nje. Ni mwiko kusema mambo hayo kwa watu ambao hawakupitia au hawakuchezewa nyimbo za msondo na kupewa mafunzo hayo.Vilevile, humfunza mwari kwamba mambo ya nyumbani kwake na mumewe haifai kuyatoa nje, anafaa kuyahifadhi kwani maisha ya mume na mke yanahitaji siri.

4.4. Uchambuzi wa Maudhui ya Nyimbo za Msondo Yasiyohusiana na Unyumba

4.4.1 Kuonyesha Nafasi ya Mungu katika Jamii

Mtafiti alishuhudia ya kwamba kabla nyimbo za msondo kuanza kuimbwa lazima wahusika wamuombe Mungu ili kufanikisha shughuli hiyo, kumaanisha kwamba wanamtanguliza Mungu kwanza. Mbali na kumtanguliza Mungu pia wanaamini ya kwamba kuna mizimu katika maisha ya binadamu na vilevile wana nafasi yao katika jamii na pia huweza kushirikishwa katika shughuli za kijamii. Mtafiti aliweza kupata wimbo huu,

Wimbo wa 15

Lala magare tuombere mlungu, tuombere mlungu	Lala magare tuombe Mungu
Ayeni ainukire	Wenzenu wainuke
Lala magere tuombere Mlungu	Lala magare tuombe Mungu
Wageni wainukire	Wageni waenukie
Aeeeh aeeeh aeeeh x3	Aeeeh aeeeh aeeeh x3

Mlungu ni Mungu na wanachama wanamuomba. *Wageni wainukire* humaanisha mizimu iliyopo pia hukaribishwa katika sherehe hii ya msondo.

Nyimbo hii husasan huimbwa wakati wa ufunguzi wa nyimbo za msondo, hii ni kama dua kwao na kutaka shughuli ifanikiwe kusiwe na mitafaruku ya aina yoyote ile. Kabla ya kuanza ngoma hii, wahusika hupiga makofi, kufagia chumba, kutia ubani ndipo sasa nyimbo za ufunguzi ziliweza kuanza na shughuli nyingine kuendelea.

4.4.2 Kuimarisha Mila na Desturi

Nyimbo hizi huhushiswa na ada tofauti ambazo hupewa mkurugwa na vilevile kwa kungwi mkuu anayemsimamia bi. harusi. Ada hii huweza kujumlisha pesa, gora za leso takribani gora kumi, seti ya vikombe, madera na kadhalika. Ada hizi vilevile zategemea ni chama kipi cha msondo kilichopewa jukumu la kupiga na kuimba nyimbo za msondo. Chama cha

Magumbakusenga huwa ghali mno lakini ukiangalia kwenye ngoma, nyimbo na mafunzo yao huchangamsha zaidi kuliko chama cha Omo.

Wimbo wa 16

Navoya Mshomoro niombole ndembo yangu x 3 Naomba ufunguo nifungue mzigo wangu

Aeee ! *Aeeeh*

Sasambu sasambu aeeeh sasambura turore Sasambu sasambu aeeeh sasambura tuone

Nakupha Mshomoro uombole ndembo yako x2 Nakupa ufunguo ufungue mzigo wako

Aeee ! *Aeeeh*

Wimbo huu huimbwa ili wahusika wapewe ada yao kabla ya kufanya shughuli yoyote ya Msondo. Neno *funguo* linaashiria ada inayohitajika kabla shughuli fulani kuendelea.

4.4.3 Kupeana Tahadhari

Mtafiti alipata nyimbo ambazo huimbwa kutahadharisha jamii kwamba lazima katika maisha mtu ajitahadharishe na watu. Binadamu hafai kuwaweka watu karibu sana kwani hajui mbaya wake ni nani, ambaye wakati wowote aweza kumdhuru, kama Waswahili wanavyosema kwamba, kikulachao kinguoni mwako.

Wimbo wa 17

Kanipiga ukuni wa utanda niko jikoni napika

Hainama nainuka damu ya tiririka

Kwa D.C ni mbali kwa chairman nitakwenda

Iyayaya wee! wabaya twawatambua

Kanipiga ukuni wa utanda niko jikoni napika

Nikainama na kuinuka damu ya tiririka

Kwa DC ni mbali kwa chairman nitakwenda

Iyayaya wee! Wabaya twawatambua

Mwanamke analalama kwamba mtu fulani amempiga akiwa akipika hadi damu zikamtoka. Hawezi kwenda kupeana taarifa kwa serikali kwani ni mbali mno lakini atakwenda kwa mzee wa mtaa kushtaki kwani anamjua aliyemfanyia ubaya huo. Wimbo huu humfunza mwari na wanajamii kwa jumla kuwa waangalifu katika maisha yao na kwamba wanafaa kutambua kwamba sio watu wote ambao wanacheka nao huwa na nia nzuri wengine waweza kuwa ndio maadui zake wakubwa.

4.4.4 Kitambulisho cha Jamii

Nyimbo za msondo zimekuwa ni kitambulisho cha jamii ya Wadigo, kwani jamii nyingi hutumia ngoma wakati wa sherehe kadha wa kadha katika jamii hizo. Nyimbo za msondo hupigwa na jamii nyingi za pwani ya Afrika.

Kwa mfano, mtafiti aligundua ya kwamba kuna nyimbo za msondo katika jamii ya Wapemba na Wabajuni. Mbali na kuwa kuna nyimbo hizi za msondo kutoka jamii moja hadi nyingine, tofauti zake zinajidhihirisha wazi.

Kwa mfano, jamii ya Wabajuni hupiga ngoma hii usiku na huwa kuna mchanganyiko wa wanaume na wanawake kwenye mduara na hawana mavazi maalum. Kwa hivyo, jinsi nyimbo hizi za msondo zinavyoimbwa na kuchezwa, jamii ya Wadigo huweza kujitambulisha kwani wanajua sheria zinazoambatana na nyimbo hizi za msondo wa Wadigo tofauti na nyimbo za msondo wa jamii nyingine.

4.4.5 Kuburudisha

Mtafiti aligundua kwamba nyimbo za msondo huburudisha wanajamii katika sherehe za harusi, ukizingatia mapigo yake yanayovutia. Wanajamii ijapokuwa si wanachama wa msondo iwapo kuna nyimbo za msondo katika harusi utawapata wanacheza nje. Vilevile utapata wanawake wengi wanajua angalau nyimbo mbili au tatu za msondo ijapokuwa wengi wao hawajui maana ya nyimbo hizo.

Wimbo wa 18

Mneemo eeeh mneemoeeeh

Nanenerwa na somu yangu mneeemo

Nanenerwa na somu yangu mnemo nakunenerwa

Mneemo ni hali ya jambo kwenda kombo au kukoseka na *kunenerwa ni hali ya* kurekebisha jambo au tabia isiyofaa.

Wimbo huu huimbwa ili kujiburudisha kwa kushirikisha wahusika na kuonyesha umuhimu wa somu katika maisha ya wanawake wa jamii ya kidigo. Jukumu la somu ni kufunza na kurekebisha tabia za wanawake huhusan tukizingatia masuala ya ndoa

Kutokana na mifano ya nyimbo tulizozipata, ni dhahiri kwamba zina mafundisho kwa yule mwari ambaye bado hajaingia katika ndoa. Aidha ni vigumu kwa mzazi wa kike au kiume kumueleza binti yake kuhusiana na masuala ya ndoa. Wazazi wanaweza kwa kiwango fulani lakini masuala kama vile kujamiiana ni vigumu kwa mzazi kuyafafanua kinagaubaga kwa mwanawe. Katika hali hii, makungwi ndio hupewa jukumu hili la kumfundisha mwari masuala yote yaliyohusiana na ndoa bila kuficha ukweli uliopo.

Watafitiwa wanaume walikiri kwamba wanawake ndio uti wa mgongo wa jamii na wao wana jukumu kubwa katika kudumisha ndoa kuliko wanaume. Na iwapo watafunzwa jinsi ya kuishi na mume, kutatua shida za ndoa basi hakutakuwa na matatizo mengi katika jamii.

Matokeo haya ya maudhui ya nyimbo hizi za msondo yaliafikiana na maoni ya Sayfa (2007) ambaye alieleza kwamba iwapo nyimbo za harusi zitatumika vizuri zinaweza kuwa chachu muhimu katika kujenga maadiqqli katika jamii na kujipatia maendeleo.

4.5 Uchambuzi wa Miiko iliyofungamanishwa na Nyimbo za Msondo

Miiko ni sheria zinazofungamanishwa na nyimbo za msondo. Utafiti huu uligudua kwamba nyimbo hizi za msondo huwa zina sheria nyingi ambazo lazima wahusika wa nyimbo hizo

wazifuate. Data iliyokusanywa iliazimia kujua iwapo watafitiwa wanafahamu miiko hii inayohusishwa na nyimbo hizi za msondo au la.

Kielelezo cha 2: Miiko iliyofungamanishwa na Nyimbo za Msondo



Data iliyokusanywa na mtafiti ilionyesha wazi kwamba asilimia thamanini ya makungwi watu wazima ambao hushiriki katika shughuli hizi walielewa miiko iliyofungamanishwa na nyimbo hizi za msondo. Asilimia ishirini ya makungwi wachanga ambao hawajabobea katika kazi hii wanafahamu baadhi tu ya miiko hii iliyotumiwa katika shughuli hizi za msondo ilhali miiko mengineo hawaifahamu.

Asilimia hamsini ya wanawake walioko katika ndoa ambao walichezewa nyimbo za msondo wanafahamu miiko hiyo ilhali asilima arubaini ya wanawake hawa walifahamu baadhi ya miiko hiyo na asilimia kumi hawakufahamu miiko hiyo.

Asilimia hamsini ya wanawake katika ndoa ambao hawakuchezewa nyimbo za msondo walifahamu tu baadhi ya miiko hii ilhali asilimia hamsini hawakufahamu kabisa miiko hiyo.

Asilimia arubaini ya wanaume walifahamu baadhi ya miiko hii iliyofungamanishwa na nyimbo za msondo na asilimia sitini hawafahamu miiko hiyo.

Miiko iliyofungamanisha na nyimbo za msondo ni mingi ila ni vigumu kupata miiko hii. Hii ni kwa sababu kuna dhana kwamba kuna mambo fulani ambayo mtu hafai kuyasema kuhusiana na nyimbo hizi za msondo.

Mtu atakayesema miiko hii alitiwa uoga kwamba pindi utakaposema, basi utarukwa na akili au ugongwe na gari na kufariki. Hali hii iliwatia hofu watafitiwa na walishindwa kusema mambo fulani waliyoyajua kuhusiana na miiko iliyohusishwa na nyimbo za msondo.

Hali hii ndio iliochangia utafiti kuonyesha kuwa asilimia thelathini na mbili ndio walifahamu miiko hii, asilimia thelathini na saba walifahamu baadhi tu. Mwishowe asilimia thelathini na mbili hawakufahamu kamwe. Watafitiwa waliofahamu miiko hii kwa kirefu ni makungwi.

Mtafiti aliweza kukusanya baadhi ya miiko hii kutoka kwa watafitiwa.

4.5.1. Uhusika katika Nyimbo za Msondo

Ni mwiko kwa mtu yeyote kufuata shughuli za msondo iwapo si mmoja wa wahusika. Kile chumba kilichopigwa na kuimbwa nyimbo hizi za msondo hujumlisha wanachama wa msondo, mwari anayepigiwa msondo na makungwi. Wanawake waliochezewa nyimbo za msondo wakati wa harusi zao wanaruhusiwa kuingia kama somu yake ni mmoja wa makungwi waliomo ndani ya chumba hicho.

Hakuna mtu yeyote mwingine aliyeruhusiwa kuingia chumba hicho ambapo shughuli hizi zinaendelea. Bi. harusi huwa na wakati maalum wa kuletwa katika chumba hicho ili kuonyeshwa mizungu. Vilevile, ikiwa mhusika mmoja anataka kuingia chumbani humo ikiwa ngoma imeshaanza basi huingia akiimba wimbo ufuatao ndio apewe ruhusa ya kuingia.

Wimbo wa 15

Nipite pii x2

Hapa miba hapo mchongoma

Nikaangalie unyago

Pita ukipenya kama uzi na sindano (kiitikio)

Kwa hivyo, huimba hapo nje hadi watu watakaposikia mule ndani ndipo atajibiwa.

Pita ukipenya kama uzi na sindano

Kumaanisha apite aingie ndani lakini asivuruge kinachoendelea kwa wakati huo. Mhusika ataingia ndani na kufuata masharti yote yanayohusiana na nyimbo hizi kwani lazima aweze kuwa mmoja wao.

4.5.2. Vyeo vya Wahusika wa Msondo

Mtafiti aligundua kwamba wahusika wa msondo wamegawanyika kimakundi kutokana na elimu waliyopokezwa kuhusiana na maswala ya ndoa. Kwanza, lazima mtu ajulikane kwamba alichezewa ngoma ya msondo wakati wa harusi yake, ndipo apate daraja la kwanza aitwe mwari. Mwari atakuwa akiandamana na kungwi wake katika sherehe za msondo hadi pale atapokezwa wari na kuvuka daraja la kuwa kungwi.

Daraja la pili ni makungwi ambao huwa wanawapa wari mafunzo ya ndoa. Cheo cha kungwi hutegemea umepitisha wari wangapi katika mafunzo ya ndoa. Kungwi akiwa amepitisha wari wengi, cheo chake kitakuwa cha juu zaidi kuliko yule ambaye amepitisha wari wachache. .

Daraja la tatu ni kungwi aliyefundisha wari ambao sasa pia wamevuka daraja la kuitwa kungwi. Hawa wanawadhifa wakupiga ngoma za msondo na huitwa Sogoro. Kufika daraja hili ni pale ambapo kungwi hupelekwa mwituni na kufundishwa mambo mengine kuhusiana na ukungwi huo na walimu wa kufunza haya ni manyakanga.

Daraja la nne tulipata mkurugwa au nyakanga huyu ndiye kungwi mkubwa anayeheshimika zaidi katika sherehe za msondo. Huyu ni kungwi ambaye aliwafundisha makungwi kadha wa kadha na sherehe yoyote ya msondo haifanyiki hadi yeye kutanguliza sherehe hiyo.

Mkurugwa ndiye anayejua masharti yote ya ukungwi na matambiko yote yanayohitajika kufanyika. Vilevile, yeye ndiye ana jukumu la kuwavukisha makungwi kutoka hatua moja hadi nyingine. Anapozungumza, watu hunyamaza na kumsikiza huku wameinamisha vichwa chini na iwapo mtu atamsalimia lazima aende kwa magoti hadi alipokaa na kumbusu mkono wake. Makungwi wakubwa ndio huwa na nafasi ya kuzungumza naye, mkurugwa huwa ni watu wazima sana kiumri.

Kuvuka daraja moja hadi jingine huwa kuna mafundisho ya aina yake na matambiko ya kumuwezesha mwari au kungwi kufikia hatua nyengine.

4.5.3 Dhana ya Kisima

Mtafiti aligundua kwamba kuna dhana inayojulikana kama kisima. Kisima hiki hutumika kuinika wari iwapo watapelekwa kwa mkurugwa na kungwi kabla ya sherehe yenyewe ya harusi na kutapishwa na matapishi huingia katika kisima hicho au shimo hili.

Baadhi ya makungwi waliohojiwa walikiri kwamba katika nyumba za mkurugwa au kungwi wakubwa wazoefu waliobebea katika kazi hii ya ukungwi huwa kuna hicho kisima. Aidha, ni shimo refu mno ambalo hufanyika matambiko kadha wa kadha yanayohusiana na nyimbo hizi za msondo.

Vilevile, ngoma za msondo hukaa ndani ya chumba hiki kilicho na kisima na hazitoki hadi ikiwa kuna sherehe ya ngoma ya msondo. Shughuli nyingi ambazo hufanywa katika chumba hiki hazijulikani na watu wa kawaida, hata makungwi wenyewe, wanafahamu mambo kidogo tu kuhusiana na chumba hiki. Sababu kuu ni kwamba kuna daraja ambalo kungwi lazima alipitie ndipo aweze kuwa mkurugwa na kuhusishwa katika shughuli hizo za kisima.

Ni vigumu sana kukutana na wakurugwa hawa kwani huwa na wasaidizi wao ambao ni makungwi. Yaliyotendeka kwenye kisima hicho ni mwiko kuyazungumzia hali ya kwamba mtafiti hakuweza kupata habari zaidi kuhusiana na dhana hii ya kisima.

4.5.4 Ngoma za Msondo

Msondo hujumlisha ngoma tatu, ngoma moja fupi iitwayo vumi na ngoma nyingine mbili ndefu zinazoitwa msondo. Ngoma hizi huwa na masharti mengi, kwanza ni mwiko kwa ngoma hizi kubebwa wazi na hufunikwa leso wakati wote isipokuwa wakati zinapopigwa ndani ya chumba.

Ngoma hizi hushikwa na watu maalum wanaojua kuzipiga na iwapo mshirika mmoja alitaka kuishika, lazima alipe ada fulani kwa mkurugwa. Vilevile, zinapopigwa, sogoro huwa ameiambatanisha ngoma hiyo na mwili wake kwa kuikumbatia tumboni kisha kufunga leso hadi nyuma kiunoni ili ngoma hiyo isianguke. Baada ya muda fulani ngoma hii hupokezwa kwa masogoro wengine ambao wataendelea kupiga ngoma hizi kwa zamu hadi sherehe ya nyimbo ya msondo itakapokwisha.

Vumi nayo huwa ngoma fupi ambayo huwekwa katikati ya miguu huku ikipigwa. Sogoro anapopiga ngoma, huwa na milio tofauti, ni wanachama tu wanajua maana ya kila mlio wa ngoma hiyo na huweza kusema ni wimbo gani utafuata na pia ni wakati wa hatua gani ya kufanyika kwa jambo fulani.

4.5.5 Kanuni ya Mavazi

Wahusika wote katika chumba kinachochezwa nyimbo hizi za msondo huwa wamevaa kanga mbili aina ya kisutu wanazoziita ndambwi, cha rangi nyekundu na sidiria pekee. Wengine wao pia hukosa kuvaa chupi. Kipande kimoja cha leso hufungwa kifuani na hakipiti magotini na kipande kingine hukunjwa na kufungwa kiunoni.

Vilevile, hakuruhusiwi kabisa kujifunika kichwa kwa hivyo, vichwa huwa wazi wakati wote wa kuchezwa nyimbo hizo na pia washiriki hawavai viatu. Washirika waweza kuwa wamejipodoa na kujiremba kwa mikufu, bangili, pete na vitu vinginevyo vya kujiremba. Ni mwiko kuingia chumba hicho iwapo hujavaa mavazi haya.

4.5.6 Matendo katika Msondo

Matendo yote ndani ya chumba hicho cha msondo hufanywa huku mikono imewekwa nyuma. Kila kitu hufanywa kwa kutingisha kiuno na kama ni kuchukua na kupeleka kitu fulani basi hufanywa kwa mdomo. Hakuna uzungumzi wa aina yoyote, mazungumzo ni ya kuimba nyimbo pekee na kucheza.

Mtu yeyote aliyetaka kuzungumza na mkurugwa basi sharti amwendee huku akitambaa kwa magoti. Uchezaji ni wa aina yake, watu huwa wako kwenye mduara na ngoma ikianzwa, huwa wanapeleka mguu mmoja mbele na mwingine nyuma huku wakizunguka. Watu wote huenda sawasawa kabla ya kuchanganyika kwa ngoma ndipo watu wanapoanza kukata viuno.

4.5.7 Mizungu

Mizungu inayofunzwa bi. harusi haifai kusemwa kwa mtu yeyote, hususan yule ambaye hakuchezewa nyimbo za msondo. Mizungu hii hufunzwa kutumia vifaa tofauti tofauti na jambo la muhimu ni kwamba mwari aweze kunengua kiuno chake akiwa katika hali yoyote au sehemu yoyote.

Kwa mfano, mwari huonyeshwa mti uliofungwa ushanga na hutakiwa aufungue ushanga huo kutumia mdomo wake, mikono ameiweka nyuma na huku ananengua kiuno hadi autoe ushanga huo kwenye mti huo.

Vile vile, ushanga huweza kuwekwa ndani ya beseni la maji na mwari akatakikana kucheza huku akiutoa kutumia mdomo wake**.** Mbali na hali hii, makungwi katika msondo hucheza

nyimbo fulani wakiwa wawili wawili huku wakimuonyesha mwari mitindo tofauti inayofanywa wakati wa tendo la ndoa.

Wanachama vilevile hushindana wao kwa wao kuonyeshana mizungu tofauti tofauti na huingia ndani ya mduara mmoja mmoja au wawili wawili ili kuonyesha au kupimana nguvu.

4.5.8 Ada za Msondo

Ada zilizotozwa kwa wanachama wa msondo ili wamchezee bi. harusi nyimbo na kumpa mafunzo hazijulikani na huwa hazisemwi, anayejua ni mkurugwa na mama au shangazi wa bi. harusi aliyeitisha ngoma hiyo. Ada za kijumla ndizo zilizojulikana kama vile kupewa cha mchana hususan kwa kungwi mkuu na mkurugwa ambapo lazima kuwe na kitoweo cha kuku.

Saa kumi lazima wapatiwe chai, lazima kutolewe gora za leso, senti za kufungua begi la bi. harusi na baadhi ya vitu alivyoletewa bi. harusi hugawanya na kungwi mkuu. Siku saba ambazo kungwi mkuu atakuwa akimwangalia bi. harusi atakapokuwa kwake pia kuna ada yake atakayopewa.

Watafitiwa makungwi waliohojia walikiri kuna ada nyingine zinazopewa kungwi lakini ni mwiko kwa wao kuzitaja kwa mtu ambaye hahusiani na nyimbo za msondo.

4.6 Uchambuzi wa Athari ya Nyimbo za Msondo katika Jamii

Watafitiwa waliohojiwa waliweza kubainisha kwamba maudhui yanayojitokeza katika nyimbo za msondo na mazingira yake yameleta athari chanya na hasi katika jamii hii ya Wadigo. Mtafiti aliweza kukusanya data hii kuhusiana na athari za nyimbo hizi za msondo katika jamii hii ya Wadigo.

Kielelezo cha 3: Athari zinazohusishwa na Nyimbo za Msondo



Kulingana na data iliyokusanywa na mtafiti ilionyesha kwamba, asilimia sabiini ya makungwi walikiri kwamba nyimbo za msondo zina athari chanya katika jamii iwapo zitatumiwa vizuri ilhali asilimia thelathini walisema kwamba nyimbo hizi zinaleta athari hasi katika jamii.

Asilimia sitini na saba ya wanawake katika ndoa waliochezewa nyimbo za msondo wanakiri kwamba nyimbo hizi na mafundisho yake yanaleta athari chanya katika jamii na asilimia thelathini na tatu ya wanawake hawa wanakiri kwamba kuna athari hasi katika nyimbo za msondo na mafundisho yake yanayoathiri jamii hii.

Asilimia arubaini ya wanawake katika ndoa ambao hawakuchezewa msondo wanakiri kwamba nyimbo hizi na mafundisho yake yana manufaa. Hii ni kwa sababu waliona kwamba kuna mambo mengi yaliyofanywa na wenzao waliochezewa msondo ambayo wao hawana habari kuyahusu kama vile kutunga vikuba vya asumini. Asilimia sitini ya wanawake hawa wanakiri kwamba nyimbo hizi za msondo na mafundisho yake yana athari hasi katika jamii.

Asilimia ishirini ya wanaume katika ndoa wanakiri kwamba nyimbo hizi za msondo na mafundisho yake yana athari chanya katika jamii na asilimia thamanini wanakiri kwamba nyimbo hizi za msondo na mafundisho yake yalileta athari hasi katika jamii.

4.7 Athari Chaya zilizohusishwa na Nyimbo za Msondo

Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa jamii ya Wadigo ina mitazamo tofauti kuhusiana na athari za nyimbo za msondo. Asilimia arubaini na tisa ya watafitiwa walisema kwamba nyimbo hizi zina athari chanya ilhali asilimia hamsini na moja walikiri kuwa kuna athari hasi zilizohusishwa na maudhui ya nyimbo hizi za msondo**.**

4.7.1 Kuhifadhi Historia

Nyimbo za msondo huhifadhi historia ya wanajamii. Hii ilijitokeza wakati ambapo mambo kadha wa kadha hufanywa wakati wa nyimbo hizi. Kwa mfano, tukizingatia historia ya jamii hii ya Wadigo, mwari alikuwa anapelekwa kwa kungwi mwezi mmoja au miezi miwili kabla ya harusi.

Mwari alikuwa anakaa huko kwa kungwi ili kupewa mafunzo yote kuhusiana na mambo ya unyumba, lakini kwa sababu ya mabadiliko katika jamii na gharama ya maisha kupanda, si rahisi kuona mwari amepelekwa kwa kungwi kukaa muda huo wote.

Mafundisho haya yamefupishwa mno, wakati wa sasa mwari hupelekwa kwa siku zisizozidi tatu au kungwi kuletwa nyumbani kwa mwari kwa masaa machache kila siku kwa takriban wiki moja hivi. Mambo yale yaliyokuwa yakifanywa hapo awali bado yatafanywa muda tu ndio utakuwa umepungua wa kutekeleza mafunzo hayo.

Hali hii iliwasaidia wanandoa kujua mambo ambayo yalikuwa yakifanywa hapo awali na bado yana umuhimu wakati wa sasa. Kwa mfano, historia kuhusu mapishi ya jamii ya Wadigo kama vile kufundishwa kupika ufuta unaoweza kuliwa na mihogo, vilevile kupika sima ya bada ambayo ni sima ya unga wa muhogo.

Vilevile nyimbo, zinazoimbwa bado ni zile zile hazijabadilika na maudhui bado ni yaleyale. Katika hali hii, tunaona ya kwamba historia hii ya Wadigo bado inaendelezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

4.7.2 Kudumisha Mila na Desturi

Nyimbo za msondo huchukuliwa kama sehemu ya unyago katika jamii ya Wadigo. Elimu hii ya unyago inamfanya kijana kujiandaa na maisha ya utu uzima.

Nyimbo za msondo hupeana mafunzo kwa wanawali kuhusu mila za jamii ya Kidigo hususan wakati wanataka kuingia katika masuala ya ndoa. Mila hii ya msondo hutekelezwa na watu wazima katika jamii. Watu hawa ni kina mama na humfunza mwari kuwa amekuwa mwanamke na kumueleza nafasi na majukumu ya mwanamke katika jamii na vilevile jinsi ya kuishi na mume.

Mila hii ya nyimbo ya msondo imekuwa ikibadilika tukilinganisha jinsi ilivyokuwa hapo awali na wakati wa sasa. Kwa mfano, hapo awali msichana alipokuwa amevunja ungo alipelekwa kwa somo kwa mafundisho ya kuingia katika utu uzima kwa takriban mwezi mmoja. Mwari alipotoka au kuhitimu ndipo alikuwa akipigiwa na kuchezewa nyimbo hizi za msondo.

Mwari huyo alikuwa hajapata mchumba lakini kwa sababu ya maendeleo ya kijamii na usasa, mwari hufunzwa na kupigiwa nyimbo hizi za msondo wakati anapotaka kuolewa na kufunzwa mila hizi na desturi za jamii ya Wadigo hususan katika masuala ya ndoa.

Kwa mfano, ni mila ya jamii ya Wadigo kutandika leso kitandani wakati mwari ameolewa na katika maisha yake ya ndoa, vilevile, mume kujifunga leso ya mkewe baada ya kuoga, kuosha mwiko baada ya kupika chakula kwani kimila ya jamii ya Wadigo mwiko uliopikiwa chakula haufai kulala mchafu ni makosa makubwa sana kwani hufananishwa na kutomsafisha mume baada ya kufanya kitendo cha ndoa.

Mila hizi huwafanya wanandoa kuwa na fahari ya jamii yao na vilevile kuwa tofauti na watu wa jamii nyingine. Kwa mfano mke katika jamii hii lazima aweze kuwa na kipepeo na makawa. Kipepeo huwa ni cha kumpepea mume na huwa kimesukwa kwa minyaa ilhali makawa huwa ni aina ya kifaa cha kufunikia chakula na pia huwa kimesukwa na minyaa.

Hutampata mwanamke wa Kidigo anayefuata mila yake akifunika chakula na kitu kingine isipokuwa makawa haya na vilevile huweza kutumika katika kupamba nyumba kama vile kuviweka sebule kwani huwa na rangi ya kupendeza na maandishi ya mipasho. Vifaa hivi huletewa bi. harusi na kungwi wake na pia mashangazi zake.

4.7.3 Ushirikiano katika Jamii

Nyimbo za msondo huleta ushirikiano katika jamii kwani wanachama wa msondo ndio waliopewa jukumu la kumfundisha mwari mambo ya unyumba ili adumishe ndoa yake. Iwapo ndoa zitaimarika, basi jamii nayo itaimarika na kizazi kitakachofuata pia kitaimarika kwa kuwa na maadili mazuri katika jamii. Katika swala la maadili mema katika jamii, ni lazima jamii iwe na ushirikiano mwema.

Ushirikiano huu husaidia wanandoa kwani wakati huu wa harusi, maharusi huletewa zawadi kama vile vyombo vya jikoni, leso, shuka na hata nguo hususan bi. harusi ambazo huweza kuanzia maisha yake ya ndoa.

4.7.4 Kufunza Maadili katika Ndoa

Mtafiti aligundua ya kwamba nyimbo za msondo hufunza maadili katika ndoa hasa tukifuata masuala ya unyumba. Masuala ya kujamiiana yameachiwa makungwi kutekeleza jukumu hili la kumfunza mwari mambo yote kuhusiana na ndoa. Makungwi hawa humfunza mwari maadili ya ndoa kwa mfano, usafi wa mwili na mazingira, kumuheshimu mume, kuwa mnyenyekevu na mstahamilivu, kujistiri kama mke wa mtu na mengine mengi. Baadhi ya maadili haya katika ndoa ni kama yafuatayo.

4.7.4.1 Kuheshimu Ndoa

Mwari hufunzwa jinsi ya kuheshimu ndoa yake kwa kujistiri kila atakapokwenda ili na yeye aheshimiwe kama mke wa mtu, alifunzwa asiwe akiambatana na wanaume ambao sio maharimu wake. Anapotoka kwake nyumbani basi afanye haraka kurudi nyumbani kwake baada ya shughuli zake na asiwe anazurura bure bila ya sababu yoyote. Mwari alifunzwa kuficha siri zake za ndani na kwamba hata kama alikumbana na matatizo katika ndoa yake haifai kuyatangaza kila mahali.

Vilevile, mwari alifunzwa kumuheshimu mume kwani ndiye kichwa cha familia na kumuomba ruhusa ya kila kitu. Kwa mfano iwapo mke anataka kwenda mahali ni sharti amuombe mume ruhusa na iwapo mumewe atakataa, basi hana budi ila kumtii mumewe na kutokwenda huko alikotaka kwenda.

4.7.4.2 Uvumilivu katika Majukumu Mazito ya Ndoa

Mwari alifunzwa kwamba katika ndoa, lazima aweze kuwa mvumilivu kwani ndani ya ndoa huwa kuna misukosuko mingi. Uvumilivu unajitokeza kwa njia tofauti, kwa mfano, uvumilivu katika hali ya maisha kiuchumi ikiwa mume ana pato ndogo mke asiwe mwenye kutaka mambo makuu ambayo mumewe hawezi kumtimizia kwa sababu ya hali yao ya kiuchumi.

Wari wanafunzwa kutoitisha talaka kila mara wanapoteta na mumewe. Wanahimizwa kujifunza kusamehe, kwani wanaume ni wale wale na kwamba tabia zao ni sawa na kuwa iwapo atatalikiwa na kuja kupata mume mwingine asidhanie kwamba watakuwa tofauti kwa hivyo atulie kwa mume aliyempata.

Mke vilevile anafunzwa kwamba anatakikana kukubali makosa na kuomba msamaha kwa mume hata kama hajafanya kosa. Kuwa na lugha ya upole mbele ya mume, kutunza watoto, kupokea mzigo wa mkubwa wake anapomuona amebeba na hasa mume kumpokea anapoingia ndani.

4.7.4.3 Kumridhisha Mume

Mwari hufunzwa jinsi ya kutunza ndoa yake kwa kumpa mume mahitaji yake yote kama kumpa chakula cha ndoa na kumridhisha ili asiende kula kwingine. Tendo la ndoa ndilo linapewa kipao mbele zaidi katika maisha ya ndoa na kwamba mke lazima amridhishe mumewe katika tendo la ndoa na asimhini wakati wowote mumewe anapomuhitaji kimwili.

Hali hii ndiyo iliyofanya nyimbo za msondo kulemea sana kumfunza mwari jinsi ya kunengua kiuno na kuonyeshwa mizungu tofauti tofauti atakayoitumia mwari katika ndoa yake. Mwari vilevile alifunzwa jinsi ya kujitayarisha kabla ya tendo la ndoa na kwamba lazima akoge na kujiremba na kujipaka mafuta ya kunukia na hata kujifukiza udi.

Vilevile alifunzwa jinsi ya kumkirimu mumewe baada ya tendo la ndoa na kwamba lazima aoge baada ya tendo hilo na kuwa safi kwani iwapo mumewe anamtaka kwa mara nyingine atakuwa katika mazingira mazuri.

4.7.4.4 Usafi

Mwari hufunzwa jinsi ya kujiangalia kwa kuwa safi kimwili na kimazingira. Mwari alifunzwa kuwa wakati wote hata kama mumewe hayupo alistahili kuwa amevalia vizuri. Mwari asivae nguo za kuchanika kwa sababu mume hayupo, iwapo kutakuja wageni basi asimuaibishe mumewe kwa kuvaa vibaya.

Vilevile mwari alifunzwa kwamba anastahili kuwa na nguo za aina zote na akiwa ndani na mumewe aweze kuvaa nguo zile. Nguo kama miniskati, suruali zile za kushika za kinadada wa sasa na nyingine nyingi. Hii ni kwa sababu mumewe akiziona zimevaliwa kule nje na wanawake wengine anajua kwamba mkewe pia nguo kama hizo anavaa ili asiweze kutamani wanawake wa nje kwa sababu ya mavazi yao.

Mwari hufunzwa jinsi ya kuweka mwili wake safi, kwa kuoga kila wakati na kujipaka mafuta kila sehemu ya mwili wake. Mwili wake unastahili laini kwa ajili ya mumewe.

Mwari asiwe mwenye kujipaka mafuta usoni tu na viganjani na miguuni bali mwili wote. Vilevile, alifunzwa jinsi ya kujifukiza kwa udi na mafuta ya kunukia.

Mwari pia alifunzwa jinsi ya kuweka mazingira ya nyumba yake safi kwa kufagia kila sehemu ya nyumba yake ikiwemo chumbani mwake mwa kulala, chooni, sebuleni na jikoni. Mwanamke alifunzwa lazima arauke asubuhi sana kwa ajili ya kufanya kazi zake za nyumba kwa utaratibu ili asiwe mwanamke mchafu atakayeweza kumfukuza mume kwa uchafu wake.

Mwari hufunzwa kwamba shuka za kutandikia kitanda chake ziwe za rangi nzuri na sio nyeusi au rangi za kiza. shuka zikiwa rangi hizo, huonekana kuwa mke ni mchafu kwani mashiti haya huweza kukaa kwa mda mrefu bila ya kuonyesha dalili ya uchafu na anastahili kubadilisha mashiti hayo baada ya siku mbili.

Mwari alifundishwa pia wakati wa kutandika kitanda chake lazima shuka yake iweze kufunika mvungu wake. Hii ilisemekana ya kwamba mvungu wa kitanda unaashiria siri za ndani kwa hivyo lazima mtu afunike siri zake.

Mwari hufunzwa kufua nguo za ndani za mumewe na zake mwenyewe na mwanamke hafai kuziweka nguo hizo za ndani na atakikana azifue kila siku. Wakati wakuanika nguo hizo za ndani, mwari lazima azifunike kwa leso zikiwa ukambani. Ni mwiko kwa mtu yeyote kuona nguo hizo za ndani za mumewe na zake hususan wakiwa wanaishi na familia ya mumewe wakiwemo bavyaa na mavyaa.

Mwari vilevile alistahili kutunza na kuangalia usafi wa mumewe kuhakikisha anamtayarishia maji ya kuoga na ikiwezekana pia anatakikana mwari kumsinga mumewe kila wakati.

Mwari alifunzwa jinsi ya kumnyoa mumewe nywele zote za mwilini na kwamba ni jukumu lake kuhakikisha mumewe ni msafi. Mavazi ya mumewe pia ni jukumu lake kumfulia na

kumpigia pasi na ikiwezekana pia kumvalisha mumewe nguo na kumvua. Hali hii itadumisha mapenzi baina ya mume na mke. Kila mara mwanamume itamlazimu arudi nyumbani mapema bila ya kuchelewa kwani anajua jinsi mkewe anavyomshughulikia vilivyo. Wari wanafunzwa kwamba mwanamume ni kama mtoto mdogo na anastahili kuangaliwa na kutunzwa kama mwana mdogo.

4.7.4.5 Sauti ya Mwanamke

Mwari hufunzwa kuwa na sauti ya unyenyekevu kwa mumewe na ya kulainishwa pindi anapoitwa na mumewe au anapozungumza na mumewe. Mwari alifunzwa kuwa mwanamke anastahili kuwa na sauti ishirini na moja anapozungumza kuzingatia ni nani anayezungumza naye na wakati gani. Kwa mfano mwanamke akizungumza na marafiki zake, mashemegi zake, mawifi zake mavyaa na bavyaa anastahili kuwa na sauti tofauti tofauti ndipo kuambiwa ya kwamba anastahili kuwa na sauti ishirini na moja.

Mumewe ni wa kulegezewa sauti kila wakati watakapokuwa chumbani mwao na kumwiita majina mazuri na ya mahaba kama vile mpenzi wangu au mume wangu. Mke akifanya hivi, basi mume ataweza kumridhisha mkewe kwa kila kitu anachotaka iwapo mwanamke atajifundisha jinsi ya kutumia sauti zake ishirini na moja na kwa wakati ufaao.

4.7.4.6 Uvivu

Mwari hufunzwa kutokuwa mvivu na kwamba mwanamke ni kurauka na kufanya shughuli zake za nyumba bila kulalamika kuwa ni nyingi au amechoka kwani hayo ni majukumu yake. Mwari alifunzwa kwamba mwanamke ni kuwa na chupa mbili moja ya chai na moja ya maji ya moto kumaanisha kwamba mwanamke si wakufanya kazi moja bali ni wakufanya kazi mbili au zaidi kwa wakati mmoja.

Mwanamke sharti ajipange kwa kuekeza kwenye vifaa na vyombo vitakavyomuwezesha kutekeleza majukumu yake kwa urahisi. Hata ikiwa mke anafanya kazi anastahili kutekeleza majukumu yake ya nyumba kabla hajatoka. Hata kama ana msichana wa nyumba kuna vitu

ambavyo havifai kufanywa na msichana wa kazi kama vile kumpikia mumewe na kusafisha chumbani mwake. Mke anafaa kuyatekeleza majukumu haya yeye mwenyewe.

Mwari anapokaa katika nyumba ya familia ambapo anakaa na mavyaa, bavyaa, wifi na shemegi zake basi vilevile anafaa kufanya kazi za nyumba kama kupika. Ni makosa kwa mavyaa kuingia jikoni iwapo mkaza mwana yuko na ameketi bila kazi yoyote.

Mwari anastahili kwanza asome nyumba ile ya kwa mumewe na afahamu wanaendesha shughuli zao vipi ili na yeye aweze kuwa mmoja wao. Mambo aliokuwa akifanya alipokuwa kwao anastahili kusahau kwani ameingia katika mji wa watu kwa hivyo atende matendo kama yanavyotendwa pale kwa mumewe.

4.7.4.7 Shanga za Kiunoni

Mtafiti aligundua ya kwamba wari hufunzwa jinsi ya kutunga shanga za kiunoni kwa ajili ya starehe ya tendo la ndoa**.** Kuna sababu maaluum ya uvaaji wa shanga hizi tukizingatia mila na desturi ya jamii ya Wadigo na sio kila mtu anaruhusiwa kuvaa shanga hizi. Ni wanawake walioko katika ndoa pekee ndio huruhusiwa kuvaa shanga za kiunoni.

Kungwi humfunza mwari jinsi ya kutunga shanga za kiunoni kutumia mitindo tofauti tofauti. Kama vile jinsi ya kutunga ushanga mmoja, shanga mbili kwa pamoja au shanga tatu au nne kwa pamoja. Shanga hizi huwa na maana kulingana na kila rangi, rangi zinazotumika ni nyekundu, nyeupe na nyeusi. Ni lazima ushanga uwe ni moja kati ya rangi hizi kwani ndizo rangi ambazo zina maana na baadaye unaweza changanya na rangi nyingine zozote zitakazoongezea urembo.

Kwa mfano, ushanga wa rangi nyekundu huvaliwa wakati ambapo mwari yuko katika hali yake ya hedhi. Mume wake atajua hali hiyo kwamba hafai kutenda tendo la ndoa na mkewe hadi pale atakapomuona mkewe amebadilisha rangi ya shanga zake.

Ushanga wa rangi nyeupe huvaliwa wakati ambapo mwanamke ashamaliza hedhi yake kumaanisha kwamba tendo la ndoa linaweza kutendeka wakati wowote watakaporidhiana mke na mume. Kila mwari aliyepitia mafunzo haya lazima avae shanga katika maisha yake yote ya ndoa wakati wote.

Ni mwiko kwa mwari kuvua ushanga wake wa kiunoni. Vilevile katika hali yoyote ile ushanga huu wa kiuno hautakikani kuonekana na mwanamume mwingine. Iliaminika ya kwamba pindi mwanamume yeyote atauona ushanga ule kiunoni basi atapanda na ashki ya tendo la ndoa hususan akiwa anajua maana ya shanga za kiuno kwa mwanamke. Mbali na hayo, mwari alistahili azihifadhi shanga zake vizuri zisionekana na mtu yeyote kwake nyumbani. Mumewe tu ndiye aliyestahili kuziona.

Shanga hizi vilevile huitwa dawa ya usingizi na huaminika kuwa ni pambo kwenye kiuno cha mwanamke ambacho hupendeza na kuwa na mvuto kikivalishwa shanga hizi. Shanga huvaliwa kwa madhumuni ya kuwaongezea hamu wakati wa tendo la ndoa mke anaponengua kiuno. Vilevile, inaaminika kwamba ikipapaswa na kuchezewa na mume huwa inaongeza hamu ya kufanya tendo la ndoa hata kama wahusika walikuwa hawana hamu hiyo.

4.7.4.8 Kuzuia Kuenea kwa Utandawazi

Katika jamii ya Wadigo, makungwi hupewa jukumu hili la kuwafunza vijana wa kike kujua majukumu yao na jinsi ya kutenda tendo la ndoa. Wari walifunzwa haya ili wasishawishike kwenda kwenye mitandao kuangalia video za ngono ili kupata mafunzo hayo.

Video hizo zinazoangaliwa na vijana zimevuka mipaka kwa kuonyesha pia ngono kati ya watu wa jinsia moja. Katika hali hii, mwari hufunzwa kwamba tendo la ndoa ni kati ya mke na mume pekee na vilevile, hufunzwa mipaka ya tendo hilo la ndoa kama vile mume hafai kukuingilia kwa nyuma.

Nyimbo hizi za msondo vilevile zilimpa mwari fursa ya kuelewa tendo la ndoa bila ya yeye kuwa na tamaa ya kuangalia picha hizo za ngono mitandaoni. Mwari iwapo angekuwa ameingia katika ndoa bila kufundishwa maswala haya basi, makungwi wake wangekuwa mitandao ya kijamii inayoonyesha picha hizo za ngono zisizokuwa na mila wala mipaka.

4.8 Athari Hasi zilizohusishwa na Nyimbo za Msondo

4.8.1 Ukosefu wa Maadili

Asilimia hamsini ya watafitiwa walikubaliana kwamba nyimbo za msondo zina athari hasi, sababu kubwa ni kuwa zina ukosefu wa maadili hasa tukizingatia utaratibu uliofuatwa katika kuendeleza maudhui yake.

4.8.2 Nyimbo za Matusi

Watafitiwa wengi walieleza kwamba nyimbo hizi zimesheheni matusi mengi ndio sababu zinaimbwa kutumia mafumbo na huzungumzia masuala ya kujamiiana tu. Ijapokuwa nyimbo hizi huimbwa ndani ya chumba kilichofungwa, watoto katika jamii huweza kusikia maneno ya nyimbo hizi na kuziimba bila kujua maana. Mtu mzima akimsikia mtoto akiziimba nyimbo hizo huweza kusema kwamba mtoto fulani amekosa maadili mema.

Watafitiwa wanawake ambao walichezewa msondo walikiri kwamba matendo waliyoyafanya wakati wa msondo pia yalisheheni matusi. Wanawake hushindana kunengua viuno kimaajabuajabu na vilevile huweza kushikana wawili wawili na kuiga jinsi tendo la ndoa linavyofanywa.

Wanawake waliomo kwenye chumba hicho kilichochezewa nyimbo za msondo huwa ni wa marika tofauti tofauti. Kuna kina mama watu wazima wanaoweza kuitwa nyanya na vilevile kuna wasichana wanaoweza kuwa wajukuu wa wanawake hawa lakini hili si tatizo wanaponengua viuno huku wakikurubiana bila wasiwasi wowote.

Watafitiwa walikiri kwamba vitendo hivi vinapotendeka havifuati maadili mema kwani washiriki hawa wanaweza kuwa mama, dada, shangazi au nyanya zetu ambapo hawastahili

kunengua viuno na kuonyeshana mizungu wakati ambapo kuna marika tofauti tofauti. Hali hii huleta utovu wa heshima.

4.8.3 Mavazi ya Nyimbo za Msondo

Watafitiwa walikerwa sana na masuala ya mavazi haswa wanaume yanayohusishwa na nyimbo za msondo. Mavazi yanakwenda kinyume na jamii na dini ya Kiislamu. Wanaohusika na nyimbo hizi za msondo huwa wafuasi wa dini ya Kiislamu na huvaa kanga mbili moja kifuani na nyingine kiunoni na haifai leso hii kupita magoti, vilevile wengine hawavai sindiria wala suruali ya ndani wanapocheza nyimbo hizi za msondo.

Ijapokuwa nyimbo hizi zinachezwa ndani ya nyumba wakati mwingine huweza kutoka nje ikiwa kuna dharura na huweza kuonekana na wanajamii hususan wanaume. Hali hii huvunja heshima ya wanawake hawa kwani ni kina mama, shangazi, dada na wake za watu. Iwapo mtu wa kando atawaona wakiwa katika hali hiyo ya mavazi yao. Mavazi haya hayastahili tukizingatia sheria za dini ya Kiislamu.

4.8.4 Uasherati

Nyimbo hizi za msondo huhusishwa na uasherati katika jamii, kwanza ukizingatia yale mavazi ya leso mbili pekee kifuani na kiunoni na isipite magotini. Leso huwa ni nyepesi mno na mtu huweza kuonekana umbo la ndani. Vilevile wanawake wengine hukosa hata kuvaa suruali ya ndani wanapocheza nyimbo hizi za msondo.

Baadhi ya watafitiwa wanawake waliochezewa nyimbo za msondo ambao bado hushiriki katika nyimbo hizi walisema kwamba, wanawake hawa wanapocheza nyimbo hizi huletewa chai ambayo huwa imewekwa kungumanga. Hii ni dawa ambayo huleta matamanio ya tendo la ndoa. Lengo la kunywa dawa hii ni kwamba haya liwatoke wakati wakinengua viuno wanapocheza nyimbo hizi.

Hali hii pia ilijitokeza hadharani kwani wanawake waliochezewa msondo hucheza kwa kunengua viuno kupita kiasi wakati wa sherehe za harusi kukiwepo na ngoma yoyote ile kama vile taarab na katika sherehe hizo huwa pia kuna wanaume.

Baadhi ya watafitiwa wanaume waliweza kutoa mifano halisi ya wanawake waliochezewa nyimbo za msondo ila ndoa zao hazidumu. Hali hii inajitokeza kwa sababu milio hii ya ngoma za msondo huweza kusikika na huwarahisi kutambua nani aliimbiwa nyimbo hizi za msondo wakati wa harusi zao. Hali hii ndio iliyowafanya watafitiwa wanaume kutoa sababu ya kuwa wanawake hawa hawatosheki na mume mmoja na mwishowe hutalikiana na kuanza kupokonya waume wanawake wengine. Wanawake hawa huitwa mashangingi kwani wanajua mbinu zote za kuwateka kiakili mabwana za watu.

4.8.5 Athari ya Usagaji

Baadhi ya makungwi walioasi kazi hii ya ukungwi wanasema ya kwamba, nyimbo za msondo na uchezaji wake zinaweza kuleta athari ya usagaji katika jamii iwapo kizazi cha sasa hakitakuwa makini ya kuzingatia mafunzo yake na miiko yake.

Hii ni kwa sababu zamani hakukuwepo na hali hii ya usagaji na wahusika wa nyimbo hizi hawakuweza kuwa na fikra kama hizi. Karne hii tuliyonayo sasa kumezuka tendo hili la usagaji. Tukizingatia jinsi wanawake wanavyocheza ngoma hizi wakiashiria jinsi tendo la ndoa linavyofanyika kati ya wao wanawake kwa wanawake, basi hali hii inaweza kuleta uwezekano wa wanawake hawa kutamaniana kimwili.

4.8.6 Ushirikina

Nyimbo za msondo huhusishwa na ushirikina kwa kiasi fulani. Kwa mfano, kuna matambiko ambayo hufanywa mara kwa mara. Wakati ngoma ya msondo inapopigwa, ilisemekana kwamba ngoma ile inapopigwa hueleza iwapo mwari ni bikira au ni mke mkuu. Ni makungwi wakuu pekee ndio huweza kutafsiri milio ya ngoma hizi na kujua maana yake.

Vilevile, kabla nyimbo hizi kuanza lazima wanachama wanyamaze kwa muda fulani, wafukize chumba kwa dawa fulani za kienyeji ndipo ngoma ianzishwe.

Swala la uji uliopewa mwari wakati wa kuinikwa pia linatiliwa shaka kwani sio uji wa kawaida na huwa umechanganywa na dawa tofauti tofauti na ni makungwi wakuu pekee ndio wanaojua dawa hizi na umuhimu wake.

Dhana ya kisima pia ilihusishwa na ushirikina ijapokuwa hakuna ushahidi wa kutosha, mtafiti hakuweza kuthibithisa haya. IIisemekana kwamba ndani ya kisima hicho kuna masanamu mawili wa kiume na kike. Masuala haya hayazungumziwi na makungwi kwa sababu ya ile dhana kuwa ni mwiko na kwamba atakayeyasema yaliyoendelea ndani ya kisima hicho basi atapatwa na wazimu au kugongwa na gari na kujifia.

Kuna dhana ambayo pia ilitiliwa shaka kuwa ilihusishwa na ushirikina, watafitiwa walikiri kwamba, wakati ambao mwari alijulikana kuwa yeye bado ni bikira, basi usiku wa kukutana na mumewe huwekewa kitambara cheupe. Kitambara hicho baada ya tendo la ndoa ikiwa mwari alikuwa bikira basi kutakuwa na ishara za damu kwenye kitambara kile. Baadhi ya watafitiwa walibaini kwamba kungwi huchukua kitambara hicho na kwenda nacho na haijulikani kitafanyiwa nini kitambara kile.

4.8.7 Udhalilishaji wa Wanawake

Baadhi ya wanawake waliochezewa nyimbo za msondo walikiri kuwa nyimbo hizi huhusishwa na udhalilishaji wa wari wakati zinapogigwa na kuchezwa. Kwa mfano, wakati ambapo mwari anafundishwa jinsi ya kutegua mzungu fulani, iwapo mwari atashindwa kunengua kiuno basi ataimbiwa nyimbo za kumkashifu na kuchapwa na myugwa.

Vilevile masuala ya kuinikwa wakati ambapo lazima mwari ajulikane kama yeye ni bikira au la. Watafitiwa wanakiri kwamba huingizwa vidole kwenye uke wao ndipo ukweli wa mambo ujulikane wazi. Hali hii humvunjia mwari heshima yake kama mwanadamu.

Udhalilishaji pia unatokea katika ndoa iwapo mke atafanya makosa basi huweza kukashifiwa na kuambiwa ataitiwa wapigaji wa nyimbo za msondo. Hii inamaanisha kwamba hakupata mafunzo kamili yanayohusiana na maadili katika ndoa. Kwa hivyo, anastahili kupigiwa msondo afundishwe maadili hayo. Hali hii itakuwa aibu kubwa kwani msondo haupigiwi wanawake waliopo tayari katika ndoa, kumaanisha mwanamke huyo ana dosari.

Watafitiwa wanawake walieleza ya kuwa maudhui ya nyimbo hizi za msondo hazimfunzi mwari namna ya kujitegemea kimaisha na daima atakuwa akimtegemea mumewe kwa kila kitu kwa mfano kimavazi na lishe.

Mafunzo ya nyimbo hizi yalimuweka mwanamke kama ni chombo cha kumfurahisha mume kimwili katika kupeana chakula cha ndoa na mapishi. Hali hii ilimdhalilisha mwanamke kuwa hana mchango wowote wa maendeleo katika ndoa yake isipokuwa mambo haya mawili ya tendo la ndoa na kuangalia nyumba yake. Hali hii inamfanya mwanamke kuwa chini ya mwanamume daima. Wanawake wengi wanakaa katika ndoa zao hata kama kuna mateso chungu nzima kwa sababu ya mafundisho haya ya nyimbo za msondo kwamba mwanamke hawachi nyumba yake katika hali yoyote ile.

4.8.8 Uharibifu wa Mali

Watafitiwa walikiri kwamba wakati wa sasa jamii inataka kuonea fahari watoto wao wanapoolewa na kufanya sherehe kubwa kupita kiasi. Wakizingatia ada hizi za msondo kuna ambazo zinajulikana wazi na nyingine zisizojulikana ambazo ni mwiko kutaja gharama hizi. Kwa mfano, kuna wanachama wa msondo wasiopungua kumi na tano, kuna makungwi na kuna nyakanga.

Watu hawa huwa kila mmoja ana ada yake atakayopewa na hugharamiwa na mama harusi. Kuna gora za leso zinazohitajika, kuna vikombe, chakula cha mchana na ada ya pesa. Msondo ni kama zile bendi za muziki na yategemea na umaarufu wa chama kimoja

kinachovutia sana ndicho kinachoitwa katika harusi nyingi. Hali hii inaleta dhana kwamba nyimbo hizi za msondo zimeingiliwa na matapeli wanaotaka kujitengenezea mapato.

4.8.9 Masuala ya Kidini

Nyimbo za msondo hupigwa na kuimbwa na jamii ya Kidigo ambao wengi ni wafuasi wa dini ya Kiislamu, lakini mambo yote yanayofanywa katika msondo yanaenda kinyume na sheria za dini hii kulingana na maoni ya watafitiwa.

Kwanza ni swala la mavazi ambapo mwanamke wa Kiislamu yafaa ajisitiri mwili wake. Ngoma ikichezwa watu hawafai kujifunika kichwa ilhali mwanamke wa kiislamu wakati wote anatakikana kujifunika kichwa chake. Pili, nyimbo zinazoimbwa ni za matusi mengi na matambiko yanayofanywa. Haya yote hayastahili kufanywa katika misingi ya dini ya Kiislamu.

Hali hii ndiyo iliyowafanya baadhi ya makungwi wa nyimbo hizi za msondo kuasi vyama vyao na kuanzisha chama kiitwacho dufu. Chama hiki hufunza wari mafunzo yanayohusiana na ndoa lakini kuzingatia misingi ya kidini.

Mavazi yao ni ya stara na nyimbo huimbwa ukumbini mahali ambapo wanaume hawatawaona. Nyimbo zake huweza kuimbwa na yeyote hata watoto wanaweza kusherehekea. Kucheza kwao ni kwa kupiga makofi bila kunengua viuno.

Wahusika wa Dufu husherekea harusi kwa kuimba nyimbo ambazo hazina matusi na kungwi mmoja au wawili pekee ndio hukaa na mwari na kumfunza kuhusiana na masuala ya ndoa na jinsi ya kumkirimu mumewe.

Takriban nusu ya mafunzo yaliyofunzwa wakati wa nyimbo za msondo ndiyo hufunzwa na wanachama wa dufu tofauti ni kwamba hapa yanafunzwa kiustarabu na stara kubwa.

4.8.10 Utengano katika Jamii

Wanawake katika ndoa ambao hawakuchezewa nyimbo za msondo wanadai kwamba wao hutengwa katika jamii. Hali hii ilijitokeza pale ambapo wanawake waliochezewa msondo hujiona bora sana kuliko wanawake ambao hawakuchezewa msondo.

Hali hii huleta utengano kwani wanawake hawa hukaa pamoja na kuzungumza mambo yao kimafumbo na lugha ambayo wao pekee ndio wanaielewa hususan kukiwa na sherehe katika jamii. Pia huimba nyimbo zao ambazo wenzao hawazijui au kuzielewa na kutoa misamiati mingi ambayo wanawake wengine hawaijui.

Vilevile, katika shughuli hizi za harusi, wanawake waliochezewa msondo huweza kupewa majukumu tofauti katika sherehe hizi, pia kuruhusiwa kuingia katika sehemu tofauti ilhali wanawake ambao hawakuchezewa msondo hawapewi majukumu haya. Vilevile hushindwa kushiriki katika mila tofauti zinazofanywa wakati wa sherehe za harusi. Kama vile wimbo huu unapoimbwa wakati wa sherehe ya harusi ya kawaida.

Wimbo wa 16

Navoya Mshomoro niombole ndembo yangu x 3

Aeee !

Sasambu sasambu aeeeh sasambusa turore

Nakupha Mshomoro uombole ndembo yako x2

Naomba ufunguo nifungue begi langu

Fungua fungua tuone

Nakupa ufunguo ufungue begi lako

Huu wimbo huimbwa wakati bibi harusi ameletewa begi linalopokewa na kungwi hadharani ambapo kila mtu huweza kuona kinachoendelea. Wimbo huu ni lazima uimbwe na wale

watakaoitikia wimbo huu ni wanawake wanaoutambua hususan wale waliochezewa msondo pekee wale wanawake wengine husikiliza tu bila kujua jinsi ya kuitikia wimbo huu.

4.8.11 Kuzuka kwa Tamaduni ya *Kitchen Party*

Kitchen party ni sherehe inayofanyika wakati wa harusi ambapo ni kumzawadi bi. harusi vyombo vya jikoni atakavyotumia katika ndoa yake akiwa kwake kwa mumewe. Sherehe hii huandaliwa na wanawake pekee. Kunaweza kuwa na uwezekano wa kuwepo kwa wanaume wasiozidi watano. Vilevile, wakati mwingine, huweza kuitwa kwa mwimbaji fulani atakayewatumbuiza wanawake hawa wakiwa katika sherehe hii ya *kitchen party*. Wanawake hawa vilevile humpa bibi harusi mawaidha ya jinsi ya kuishi na mumewe katika ndoa.

Sherehe hii haina utaratibu maalum na huchukua taratibu tofauti tofauti. Kitu cha msingi ni kuwa wanawake hawa humzawadi bibi harusi mmoja baada ya mwingine na kila mmoja wao akienda kupeana zawadi yake basi huonyesha mzungu wake wakunengua kiuno. Iwapo kutakuwa na mwimbaji au kuwekwe redio na nyimbo tofauti kuimbwa basi wanawake hawa hucheza kwa kunengua viuno na huku wakimuonyesha bi. harusi mitindo tofauti tofauti ya kufanya tendo la ndoa.

Mara nyingi bi.harusi akiandaliwa *kitchen party* ni kwamba hakukuwepo nyimbo za msondo ndipo sasa mwari anapewa mafunzo hayo ya tendo la ndoa kwa mukhtasari. Hii ni kwa sababu pengine kuna ukosefu wa fedha za kuita ngoma ya msondo au wakati mwingine huweza kufanyika zote mbili *kitchen party* na nyimbo za msondo kwa siku au wakati tofauti katika siku ya sherehe ya harusi. Sherehe hii ya *kitchen party* imeleta midahalo mbalimbali ya kwamba wanawake wanaokwenda katika sherehe hizi hutaka kujionyesha tu nani aliyebora kuliko mwingine katika unenguaji wa viuno.

Mtafiti anakubaliana na maoni ya Mohammed (2015), aliposema kwamba katika kipindi hiki cha ugeni mwingi, jamii zetu zimeiga mila na desturi za kigeni ambazo huendeshea

shughuli za harusi zao kinyume kabisa na misingi ya Kiafrika. Mfano wa sherehe hizo ni *hina Party* na *kitchen Party*. Sherehe hizo hazitoi mafunzo yoyote kwa wanandoa bali ni ufakhari wa kujionesha tu na ukusanyaji wa vyombo na pesa kwa hila.

Watafitiwa wanaume waliokiri kwamba nyimbo hizi za msondo zina athari hasi wanatoa ushahidi kwa kutaja majina ya wale wanawake katika jamii ambao ni makungwi. Ushahidi wao ni kwamba wengi wa makungwi hawa ni wataliki. Hali hii inaleta mtafaruku kwamba makungwi hawa watawezaje kuwafunza wari jinsi ya kukaa na mume ilhali wao nyumba zao zilivunjika.

Kutokana na maoni ya watafitiwa, asilimia hamsini wanasema nyimbo hizi zina athari hasi. Utafiti huu ulidhihirisha kwamba athari za nyimbo za msondo kwa wanandoa ni chanya kwa sababu mwanamke anafunzwa jinsi ya kuangalia majukumu yake katika ndoa.

Mtafiti aligundua kwamba mambo mengi ya athari hasi yaliyohusishwa na nyimbo hizi hufanywa kabla ya mwari kwenda kwa mumewe kama vile mavazi na nyimbo za matusi. Mavazi yale mwari hata yavaa tena akiwa kwa mumewe na nyimbo zile za matusi hataziimba akiwa kwa mumewe bali atafuata tu mafunzo aliyojifunza kudumisha ndoa yake.

Mafunzo haya ni mazuri kama vile jinsi ya kuwa msafi, kuandaa chakula na kadhalika yanamfunza mwari kujua majukumu yake kama mke na mama. Hali hii itaifanya jamii kuwajibika katika kutekeleza majukumu haya.

Matokeo ya athari zilizohusishwa na ngoma hizi za msondo zilishabihiana na maoni ya Silau (2013), kwamba vijana wengi hawapendi nyimbo na ngoma za kitamaduni badala yake wanapenda muziki ya kisasa kwa sababu nyimbo hizi huchezwa kwa nadra sana katika jamii.

Hali hii ndiyo iliwafanya watafitiwa wengi kutojua nyimbo hizi za msondo na vilevile kueleza dhana tu kuhusiana na nyimbo hizi bila ya kuwa na ushahidi wowote. Sayfa (2007)

anaeleza kwamba matatizo yanayozikabili nyimbo za harusi ni kutokana na jamii kutoyazingatia mafundisho yake. Vilevile utafiti huu ulikubaliana na maoni yake kuwa wanajamii wa Kidigo hawazingatii mafundisho ya nyimbo hizi za msondo kwani wengi wao hawajihusishi na nyimbo hizi na iwapo jamii hii itazingatia mafundisho yake basi tutatatua dhana hasi zinazohusishwa na nyimbo hizi.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Katika sura hii, tulishughulikia mukhtasari wa utafiti, kwa kuzingatia maelezo katika kila sura, mukhtasari wa matokeo ya utafiti huu, hitimisho na mwishowe kutoa mapendekezo ya utafiti zaidi unaohitajika kufanywa katika mazingira ya nyimbo za msondo.

5.2 Mukhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu ulijumlisha sura tano, sura ya kwanza imeangazia usuli wa mada, swala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuuchagua mada, upeo na mipaka, umuhimu wa utafiti na mwishowe udhaifu wa utafiti huu.

Sura ya pili ilifafanua uhakiki wa mapitio, imehakiki kazi mbalimbali zilizoandikwa kuhusu mada hii ambazo tumezieleza jinsi zilivyochangia kufanikisha utafiti huu. Msingi wa nadharia umejadiliwa pamoja na mihimili yake iliyotumika kufanikisha kazi hii.

Sura ya tatu imeeleza mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu na maswala mengine yakijumlishwa kama vile eneo la utafiti, utaratibu wa utafiti, uteuzi wa sampili, mbinu za kukusanya data, mbinu za uchanganuzi wa data na mwishowe uwasilishaji wa data.

Sura ya nne ilijadili uwasilishaji na uchanganuzi wa data ilijumlisha uchambuzi wa maudhui ya nyimbo za msondo ambayo yalihusu unyumba na maudhui mengine yasiyohusu unyumba. Uchambuzi wa miiko iliyofungamanisha na nyimbo hizi za msondo na mwisho uchambuzi wa athari zinazohusishwa na nyimbo hizi zikiwemo athari chanya na hasi.

Sura ya tano imehitimisha kwa mukhtasari utafiti wote kwa jumla ambao tuliangazia mukhtasari wa utafiti, mukhtasari wa matokeo, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu.

5.3 Mukhtasari wa Matokeo

Mukhtasari wa matokeo ya utafiti huu ulinuia kuchunguza maudhui ya nyimbo za msondo na athari zake kwa wanandoa katika jamii ya Wadigo**.** Kuhusiana na maudhui ya nyimbo za msondo matokeo yalionyesha kwamba asilimia sitini na nane ya watafitiwa wamekiri kwamba maudhui ya nyimbo za msondo yalihusu masuala ya unyumba kama vile maadili katika ndoa, masuala ya ngono, nafasi ya mwanamke katika jamii, mila na desturi na mengineo. Utafiti huu vilevile uligundua ya kwamba asilimia thelathini na tatu ya watafitiwa walikubali kwamba mbali na maudhui ya unyumba, nyimbo hizi za msondo zimebeba maudhui mengine yasiyohusiana na unyumba kama vile nafasi ya Mungu katika jamii na kupeana tahadhari kwa wanajamii.

Matokeo ya utafiti huu kulingana na maudhui ya nyimbo za msondo yalilingana na maoni ya kazi ya Mohammed (2015), ambaye alieleza kwamba nyimbo za ngoma ya msondo ni zenye kutoa elimu na pia zilitoa mafunzo kwa maharusi na zinastahili kuendelezwa na kudumishwa.

Utafiti uligundua ya kwamba kuna miiko mbalimbali ambayo lazima izingatiwe wakati nyimbo za msondo zinapopigwa na kuchezwa. Miiko hii hutumika kuendeleza maudhui ya nyimbo hizi za msondo. Asilimia thelathini na mbili ya watafitiwa walikiri kwamba wanafahamu miiko hii. Asilimia thelathini na saba ya watafitiwa walikiri walifahamu baadhi tu ya miiko hii na asilimia thelathini na mbili walikiri kwamba hawafahamu miiko hii iliyohusishwa na nyimbo za msondo. Mifano ya miiko hii ni kama vile uwanachama, mavazi, taratibu za shughuli za msondo, ngoma za msondo na nyinginezo.

Matokeo ya utafiti kuhusu athari za nyimbo za msondo katika jamii, ulidhihirisha wazi kwamba nyimbo hizi zina athari chanya na hasi. Asilimia arubaini na tisa ya watafitiwa walikiri kwamba maudhui ya nyimbo hizi yana athari chanya kama vile kufunza maadili ya ndoa, kudumisha mila na desturi ya jamii, kuzuia kuenea kwa utandawazi, kuleta

ushirikiano katika jamii na mengine mengi yaliyojitokeza wakati wa mafundisho haya ya nyimbo za msondo. Asilimia hamsini na moja walikiri kwamba kuna athari hasi zilizojitokeza katika jamii zilizohusishwa na maudhui ya nyimbo za msondo. Athari hizi ni kama vile kufunza uasherati, kudhalilisha wanawake, uharibifu wa mali, kufanikisha ushirikina, kuvunjika kwa ndoa, ukiukaji wa masuala ya kidini, utovu wa nidhamu na mengine mengi.

5.4 Hitimisho

Utafiti huu ulinuia kuchanganua maudhui ya nyimbo za msondo na athari zake kwa wanandoa katika jamii ya Wadigo.

Utafiti huu ulithibitisha kwamba tunapata mafunzo mazuri na mengine yenye utata ambapo jamii inafaa kuja pamoja tuweze kuwa na msondo mamboleo ili kuepusha vizazi vya baadaye kuwa na familia zisizo na maadili na mbinu za kutumia kujihami kimaisha hususan katika maisha ya ndoa. Jamii inafaa kuhamasishwa kuhusu manufaa ya nyimbo hizi za msondo ili jamii hii ijionee fahari ya utamaduni wao.

Utafiti huu ulitambua kwamba kuna mambo mengi ambayo hayajulikani kuhusiana na nyimbo hizi za msondo na mafundisho yake. Utafiti huu ulikiri kwamba ulipata baadhi tu ya mambo yaliyotendeka, lakini mengine mengi bado hayajapatikana. Hii ni kwa sababu wanayoyajua hawako tayari kuyasema kwa kuwa ni mwiko kusema mambo haya ya ndani sana na wanayoyajua ni wachache sana na kuwafikia pia ni kazi kubwa.

Kuna dhana ya ushirikina ambayo ilijitokeza lakini wahojiwa walijua machache sana kuyahusu. Vilevile kuna dhana ya kisima, kila kungwi aliyehojiwa alikiri kwamba dhana hii ipo lakini hawakujua yaliyofanywa ndani ya kisima hicho na umuhimu wake ni nini. Wengine wao hawajafika daraja hilo la mwisho kujua yaliyofanyika katika kisima hicho.

Kutokana na matokeo ya utafiti huu ilionekana wazi kwamba nyimbo za msondo zina manufaaa katika jamii ya Wadigo. Tatizo kubwa ni kwamba jamii hii haijahamasishwa kuhusiana na nyimbo hizi kwa sababu ya usiri mwingi uliofungamanishwa na nyimbo hizi. Watafitiwa wengi walifahamu kuwepo kwa nyimbo hizi lakini hawajui mambo yaliyotendeka au wanafahamu baadhi tu waliyoyasikia kwa wengine na mara nyingi yale waliyosikia ni mambo ya kupotosha.

Utafiti huu ulitudhihirishia ya kwamba asilimia kubwa ya vijana hawapigiwi na kuchezewa nyimbo za msondo wakati wa harusi. Wengi wao hukosa yale maadili fiche yaliyomo katika ndoa. Tuliwaona wanawake waliochezewa msondo hujiona bora zaidi au kuwa wanawake kamili kushinda wale ambao hawakuchezewa msondo. Vilevile wale ambao hawakuchezewa pia hujiona duni na wasiojua chochote mbele ya wenzao waliochezewa msondo.

Kazi hii ya utafiti ilibaini kwamba jamii ina mtazamo hasi kuhusiana na nyimbo za msondo bila ya wao kuwa na ushahidi wa kutosha wa madai yao. Wanaume katika jamii hii hawataki kabisa mambo ya msondo na hii ni kwa sababu hawajui mambo yaliyoendelea, kwa mtazamo wao wanawake hufunzwa mambo mengi machafu.

Kila jamii huwa na mila na desturi zake za kumrukisha kijana kutoka rika moja hadi jingine. Nyimbo hizi za msondo hutumiwa kumfunza mwari mambo ya utu uzima na unyumba katika jamii hii. Sheria hizi hazipatikani katika maandishi na zitakazopatikana katika mitandao basi nyingi hupotosha vijana, ndiposa hupata watu wakitalikiana kila wakati. Tunahitaji mafunzo haya kama jamii ili kuepusha kizazi chetu na balaa za ulimwengu.

Mafunzo ya ndani ya nyumba ni muhimu sana kwa vijana wa leo kwa sababu watu hawaishi kwa pamoja kama wakati wa zamani. Jamii zimetawanyika wengine wanaishi vijijini na wengine wanaishi mijini. Wanawake wengi wamesoma na hawajui majukumu yao katika ndoa kama vile usafi, mapishi, mahitaji ya mume na mengine mengi. Majukumu haya

yameachiwa wafanyikazi wa nyumba. Ndipo sasa kila kukicha wanandoa wanatalikiana kwa sababu ambazo zinaweza kuepukika, iwapo kila mtu atajua wajibu wake katika ndoa.

Utafiti huu ulikubaliana na maoni ya Rashid (2013), kwamba mafunzo ya nyimbo za jando na unyago yana kasoro ambazo zinahitaji kufanywa marekebisho katika jamii ya Wahiyao. Vilevile katika jamii hii ya Wadigo tuligundua pia nyimbo hizi za msondo zina mapungufu kwa kiasi fulani. Jambo la msingi ni kwamba jamii ikubaliane na baadhi ya sheria hizi na zile ambazo wanajamii wanadhani zimepitwa na wakati, ni mbovu zitupiliwe mbali na zilizo bora ziwekwe na ziboreshwe.

Matokeo ya utafiti huu ulithibitisha kwamba nyimbo za msondo katika jamii ya Wadigo ni tofauti kabisa na nyimbo za kawaida za harusi katika jamii ya Wadigo. Hali hii imetokana na mtafiti kulinganisha kazi ya Ngome (2014), iliochambua maudhui na majukumu ya nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili. Nyimbo zilizochambuliwa ni tofauti kabisa na nyimbo tulizozichambua katika utafiti huu.

5.5 Mapendekezo

Utafiti huu ulitafiti maudhui ya nyimbo za msondo na athari zake kwa wanandoa katika jamii ya Wadigo. Tuligundua ya kwamba kuna mambo mengi yaliyohusishwa na nyimbo hizo za msondo mbali na yale tuliyoyapata.

Tunapendekeza kuwa tafiti zingine zifanywe kuhusu matambiko yanayohusishwa na nyimbo za msondo. Vilevile dhana ya kisima iweze kufafanuliwa kwa kina na jamii ipate kufahamu mambo yote yanayohusiana na dhana hii ya kisima ikiwemo umuhimu na majukumu yake ni yapi katika kufanikisha nyimbo za msondo.

Vilevile tuligundua ya kwamba jamii ya Wabajuni pia hucheza nyimbo za msondo kwa hivyo tunapendekeza kuchanganuliwa kwa tofauti na mfanano wa nyimbo hizi kati ya jamii ya Wadigo na Wabajuni.

Tunapendekeza vilevile watafiti wengine washughulikia nyimbo za dufu ambazo pia huimbwa wakati wa harusi kwa kuangalia mafunzo yake, utaratibu wake na umuhimu. Hii ni kwa sababu nyimbo hizi zilijitokeza wakati wa kukusanya data ya utafiti huu.

Utafiti huu ulifanywa katika maeneo ya Likoni mtaa wa Jamvi la Wageni na Migombani. Tunapendekeza utafiti mwingine ufanyike katika maeneo ya Kwale kama vile Tiwi na Ukunda kutathmini tofauti zinazopatikana ikilinganishwa na nyimbo za msondo za maeneo ya Likoni.

Tunapendekeza vilevile iwapo serikali au taasisi za kibinafsi zinaweza kutoa ufadhili kwa watafiti, ili mambo yote yanayohusishwa na nyimbo za msondo yatafitiwe na kuwekwa wazi ili jamii iweze kufaidika na pia kuongeza elimu katika nyanja ya fasihi simulizi.

Tamaduni hii ya nyimbo za msondo inaweza kudumishwa na jamii ya Wadigo waikubali bila mapungufu yoyote. Tunapendekeza makungwi hawa wapewe elimu zaidi kuhusu masuala ya ndoa na jamii ya kisasa. Elimu hii itawawezesha kuwafunza wari mambo mengi mbali na tendo la ndoa na mapishi pekee. Tunaweza kuomba usaidizi kama vile jinsi wakunga walivyopewa elimu mpya na mabadiliko ya kiteknolojia ya uzalishaji na kupewa vyeti vya kuhudumu. Vilevile makungwi wanaweza kupewa mafunzo haya kwa upana zaidi.

Mafunzo haya yalitolewa na wanawake na kueleza jinsi ya kukaa na mume na namna wanaume walivyo. Ni kinaya kwamba watu wanawachukulia mama zetu kuwa na elimu zaidi kuhusu jinsi ya kumtunza mume kutokana na tajriba walizonazo. Tunapendekeza kuwa ingekuwa vyema zaidi iwapo wanaume pia watapewa mafunzo haya kuhusu majukumu ya mume kwani wanaume wenyewe ndio wana uwezo wa kujieleza ipasavyo.

Ndoa ni ya watu wawili na ingekuwa vyema iwapo wanandoa watarajiwa wote watapewa mafunzo kuhusu suala la ndoa na asipewe mwanamke pekee. Mwanamume ambaye ataingia

katika ndoa hapewi mafunzo kama haya wanayopewa vijana wa kike. Vijana hawa wanapoanza maisha ya ndoa, basi mara nyingi kuna migongano baina yao kwa kuwa mmoja ana matarajio zaidi kwa mwenziwe kuliko mwingine. Tunapendekeza kuwa wanaume pia wapatiwe mafunzo haya ya unyumba.

MAREJELEO.

Agawu, K. (2001) African Music as Text: *Research in African Literature*, 32 (2), 8-16

Beja, S.K. (2000) Giriama Funeral Songs: Functional Aesthetic Study. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Gitonga, W. (2017) Uchanganuzi wa Fani na Maudhui ya Nyimbo za Harusi za Kimeru na Waswahili. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Hegel, G.W. (1979) *Introduction to Aeshetics*. London: Oxford University Press.

Kingei, K. (1993) Language Culture and Communication. The Role of Taarab Songs In Kenya 1963-1999. Tasnifu ya Uzamifu, Harvard University. (Haijachapishwa)

Kobia, M. (2011) Taswira ya Kiuana katika Nyimbo za Tohara za Wanaume Miongoni mwa Waigembe. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Kirubi. N. W. (2007) Dhana ya Nyimbo: Sifa, Miundo, Aina mbalimbali na Majukumu ya Nyimbo. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Makange, J.K. (2015) Ulinganishi wa Fani za Kiutendi katika Nyimbo za Harusi miongoni Mwa Jamii ya Wataveta na Waswahili. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Matei, A.K (2011) *Fani ya Fasihi Simulizi*. East Africa Ltd: Oxford University Press

Mjomba, G. (2001) Uchambuzi wa Nyimbo za Harusi za Wadawida. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Mohammed, A. (2015) Kuchunguza Dhima za Nyimbo za Msondo wa Pemba. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa).

Mogambi, H. (2007) Uchambuzi wa Nyimbo za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Mugenda, O na Mugenda A. (1999) Research *Methods: Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: Acts Press.

Njogu, K. na Chimera R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation**.**

Njogu, K. na Wafula M. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation**.**

Ngome, D.M. (2014) Uchambuzi Linganishi wa Maudhui na Majukumu ya Nyimbo za Wadigo na Waswahili. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Ntarangwi, M. (2004) *Uhakiki wa Kazi za Fasihi.* Augustana College: Rock Island, IL612, Publishers Ltd.

Peter, B. (1995) *Beginning Theory: An Introduciton to Literary and Cultural Theory.* London: Manchester University Press**.**

Rashid, H. (2013) Mafunzo ya Nyimbo za Jando na Unyango kwa Jamii ya Wahiyao wa Maasai, Tarafa ya Luhidi. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa)

Sayfa Group, (2007) Athari za Nyimbo za Harusi. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Taifa SUZA. Zanzibar (Haijachapishwa)

Silau, G. (2013) Kutathmini Dhima ya Nyimbo katika Kukuza na Kuimarisha Malezi mfano wa Kabila la Wakaguru. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa)

Spear, T.T. (1978) *The Kaya Complex*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Timammy, R (2002) Mombasa Swahili Women's Wedding Songs*:* A Stylistic Analysis. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

TUKI. (1981) *Kamusi ya Kiswahili.* Nairobi: Oxford University Press.

TUKI. (2000) *English-Swahili Dictionary.* Second Edition. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Wafula, R. na Njogu, K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2003) *Kichocheo cha Fasihi.* Nairobi: Focus Publication Ltd.

Waziri, M.M. (2016) Kuchunguza Dhima za Nyimbo za Singo katika Kijiji cha Uzini Zanzibar. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa)

Yego, K. (2013) Nafasi ya Mwanamke jinsi Inavyotetewa katika Nyimbo za Taarab za Zanzibar. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

KIAMBATISHO CHA 1

MWONGOZO WA MAHOJIANO

1. Msondo ni ngoma ya aina gani?

   ……

   ……

   ……

   ……

2. Kila ngoma huwa na taratibu zake zinapoimbwa. Je nyimbo hizi za msondo hufuata taratibu zipi?

   ……

   ……

   ……

   ……

3. Je, nyimbo hizi za msondo zinapoimbwa wakati wa harusi zinalenga kupitisha ujumbe gani?

   ……

   ……

   ……

   ……

4. Je? Nyimbo hizi zina maudhui gani katika Jamii.

   ……

   ……

   ……

   ……

5. Umuhimu unaojitokeza katika nyimbo hizi ni upi?

……

……

……

……

……

……

6. Je? Kuna athari zozote zinazojitokeza katika jamii zinazohusishwa na nyimbo hizi za msondo

……

……

……

……

……

……

7. Kuna miiko inayoambatanishwa na nyimbo hizi za msondo?

……

……

……

……

……

……

KIAMBATANISHO 2

NYIMBO

Wimbo wa 1

Baba niundie chombo nisafiri niende amu
Nikamtwae mwengereza na nduguye mkadamu
Kama si kuvunja ngome niite mwanaharamu x3

Baba nitengezee chombo nisafiri niende lamu
Nikamchukue mwengereza na ndugu yake mkadamu
Kama si kuvunja ngome niite mwanaharamu x3

Wimbo wa 2

Mtaimbo

Mwimbaji : Wateleza huo
Kiitikio : Hauna laika
Mwimbaji : Ni mwembamba huo
Kiitikio : Hauna laika
Mwimbaji : Una tundu huo
Kiitikio : Hauna laika
Mwimbaji : Ukiupeleleza mtaimbo, wateleza mtaimbo

Wimbo wa 3

Gandomfuko

Huko baharini kuna nyama,aitwa Gandomfuko
Ukitaka kula nyama, paka umfate kuko
Wende ukale nyama, gando uliriche kuko

Huko baharini kuna nyama aitwa Gandomfuko
Ukitaka kula nyama, paka umfate huko
Wende ukale nyama, gando uliache huko

Wimbo wa 4

Tamu tamu ta tate x2	Tamu tamu ta tate*x2*
Chanda na pete	Chanda na pete
Ulimi na mate	Ulimi na mate

Huo mzungu siumanyire x3 Huo mzungu sikuujua x2

Wimbo wa 5

Kunguru na mwewe watetea ndege paruanja x2

Kunguru na mwewe watetea ngege uwanjani

Wimbo wa 6

Kunguru ndege ayumba yumba Kunguru ndege ayumba yumba

Nipelekeni kwa somu nikausore mirimo x 2 Nipelekeni kwa somu nikaokote mitindo x 2

Wimbo wa 7

Nafita mzungu wangu mwari sina Naficha mzungu wangu mwari sina

Ajaliwaye naende akauchole x3 Ajaliwaye aende akauchukue x3

Wimbo wa 8

Chimba chimba x3 Chimba chimba

Makungwi arore paruwanja makungwi waone uwanjani

Wimbo wa 9

Nipeni kungu nitafune x 2 Nipeni kungu nitafune

Ni yamezee mate, nijivute Niyameze mate nijivute

Bembereze mato, kwa waume Nilegeze macho kwa wanaume

Wimbo wa 10

Mke mwenzangu mume ametwawa Mke mwenzangu mume amechukuliwa

Na atwawee mwana kutwawa x2 Na achukuliwe mwana kuchukuliwa

Na huku endako endee akatwawe x2 Na huko anakokwenda pia akachukuliwe

Na bendera yangu ninayo mwenyewe x2 Na bendera yangu ninayo mwenyewe

Wimbo wa 11

Mwimbaji *Aliniahidi huyo kishindo, ataniondoa mimi mgandamo*

Lakini silaha sijaiona, mgandamo sijaiona

Sijali mama……

Kiitikio *Sijali*

Mwimbaji *Sijali maneno*

Kiitikio *Sijali*

Mwimbaji *Sijali kusengenywa*

Kiitikio *Sijali*

Wimbo wa 12

Nipani kiribiti eeeh	Nipeni kiribiti
Nng'arire mwari	Nimng'arie mwari
Nng'a nnga' nga'rare	Nimng'arie ng'arie mwari
Mwari ng'are ng'are x3	Mwari ng'are nga're

Wimbo wa 13

Eeeeh mwari ashindwa na mzungu x 3

Wimbo wa 14

Usinende nisema x3 Mwari

Usinende nisema kama somu ana marewerewe ya matako. (Kiitikio*)*

Usiende kunisema mwari x3

Usiende kunisema kama somu ana marewerewe ya matako (Kiitikio)

Wimbo wa 15

Lala magare tuombere mlungu,tuombere mlungu	Lala magare tuombe Mungu
Ayeni ainukire	Wenzenu wainuke
lala magere tuombere Mlungu	Lala magare tuombe Mungu
Wageni wainukire	Wageni waenukie
Aeeeh aeeeh aeeeh x3	Aeeeh aeeeh aeeeh x3

Wimbo wa 16

Navoya Mshomoro niombole ndembo yangu x 3	Naomba ufunguo nifungue mzigo wangu
Aeee !	*Aeeeh*
Sasambu sasambu aeeeh sasambusa turore	Sasambu sasambu aeeeh sasambura tuone
Nakupha Mshomoro uombole ndembo yako x2	Nakupa ufunguo ufungue mzigo wako
Aeee !	*Aeeeh*

Wimbo wa 17

Kanipiga ukuni wa utanda niko jikoni napika

Hainama nainuka damu ya tiririka

Kwa D.C ni mbali kwa chairman nitakwenda

Iyayaya wee! wabaya twawatambua

Kanipiga ukuni wa utanda niko jikoni napika
Nikainama na kuinuka damu ya tiririka
Kwa DC ni mbali kwa chairman nitakwenda
Iyayaya wee! Wabaya twawatambua

Wimbo wa 18

Mneemo eeeh mneemoeeeh
Nanemerwa na somu yangu mneeemo
Nanemerwa na somu yangu mnemo nakunemerwa

Mneemo ni hali ya jambo kwenda kombo au kukoseka na *kunenerwa ni hali ya* kurekebisha jambo au tabia isiyofaa.